
Jumatano Desemba 25, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581901 MWANGA WA JAMII www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0677 020 710 LIKE & FOLLOW US
Nipashe digital

epaper.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com




UKURASA WA3

**NEMC** mguu kwa mguu na wapiga kelele Krismasi

UKURASA WA 3

**Bwana** harusi anayedaiwa kujiteka akosa dhamana kortini


UKURASA WA 18

**Samia** aunda tume mbili za kusawazisha kinachoendelea Ngorongoro

MBOWE VS LISSU...

# Lema: Maombi yataniongoza kumpata aliye sahihi CHADEMA

UKURASA 2





Mkuu wa Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, Kasilda Mgeni, akiongoza wananchi kuaga miili ya baadhi ya watu waliofariki dunia kutokana na mvua iliyonyesha wilayani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UKURASA WA 18

## MVUA YAKATA MAWASILIANO KATA TANO SAA 72

MVUA inayoendelea kunyesha wilayani Same, mkoani Kilimanjaro imesababisha kukatika kwa daraja la Kizangaze na kukata mawasiliano kati ya kata ya Maore, Ndungu, Kihurio, Bendera na kata ya Miamba kwa saa 72...

## Ajali nyingine yachukua uhai wa watu saba na kujeruhi 10

UKURASA 2


## Majambazi wazua taharuki mpakani



UK. 10

**MICHEZO** YANGA YAWAANDALIA 'WANANCHI' ZAWADI KRISMASI UK.24

**MAONI,** UK.6



Mbunge wa Musoma Vijijini mkoani Mara, Prof. Sospeter Muhongo (katikati aliyenyoosha mkono), akiwa na wakazi wa Kata ya Bugwema jimboni humo wakati akikabidhi gari ya kubebea wagonjwa lililotolewa na serikali kwa kituo cha afya cha kata hiyo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

MBOWE vs LISSU

# Lema: Maombi yataniongoza kumpata aliye sahihi CHADEMA

**Na Elizabeth Zaya**

MWENYEKITI mstaafu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema amesema atafanya maombi kwa Mungu kupata upande sahihi wa kuunga mkono katika mvutano wa kumpata mwenyekiti wa chama hicho.

Amesema muda si mrefu ataonesha ni upande gani anaounga mkono kati ya Mwenyekiti wa sasa wa chama hicho, Freeman Mbowe na Makamu wake, Tundu Lissu.

"Kwa sasa sina timu, pengine siku za usoni ninaweza kujali zaidi juu ya mwelekeo wangu kwa nani ninapenda awe kiongozi mkuu kwenye chama chetu.

"Kwa sasa ninatazama, ninafikiria na kusali, kwa sababu hii position (nafasi) wanayoomba ina umuhimu hata kwangu pia kama mwana-CHADEMA," alisema Lema.

Mbowe na Lissu wanagombea nafasi moja ya uenyekiti wa chama hicho taifa na tangu watangaze nia, kumekuwa na mvutano mkubwa mitandaoni kutoka kwa makada na wafuasi wa chama hicho wanaoonekana kugawanyika makundi mawili ya wanaomtaka Mbowe aendelee na wanaomtaka Lissu apokee kijiti hicho.

Akizungumza na Nipashe jana, Lema ambaye ni Mjumbe wa Kamati Kuu wa chama hicho alisema kuwa amekuwa mtazamaji na anafikiria kuanza kusali kabla ya kuonesha upande anaounga mkono kati ya vigogo hao wawili.

Lema alisema kuwa kikubwa anachoomba hivi sasa kwenye chama chake ni utulivu kuelekea uchaguzi huo wa ndani ya chama.

"Ninachoomba kwa sasa ni utulivu ndani ya chama, ila hata kama kuna mgombea nitamuunga mkono na kwa sababu atakuwa ni mwana-CHADEMA, sidhani kama litakuwa jambo baya," alisema.

Lema aliyewahi kuwa Mbunge wa Arusha Mjini, alitoa angalizo kwa wanachama na wafuasi wa CHADEMA kwamba katika kipindi hiki cha uchaguzi ndani ya chama, kuna haja ya kuwa makini katika kutoa majibu yanayotokana na hisia za wanachama wanaounga mkono upande wowote wa wagombea.

Vilevile, mstaafu huyo pia alitoa angalizo kwa wanaonyukana kupitia mitandao ya kijamii, akiwataka kuweka mbele maslahi ya chama chao hususani katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwakani.

"Tumetoa maazimio kuelekea Uchaguzi Mkuu mwaka kesho, kwamba 'no reforms no election' (hakuna mabadiliko hakuna uchaguzi). Tunatakiwa tuweke nguvu yetu huko, lakini endapo haya yataendelea si tu ni hatari kwa chama chetu, bali pia hata kwa nchi yetu kwa maana chama hiki ndicho kinapigania Katiba mpya na mifumo bora ya uchaguzi ambalo ndilo la msingi kuliko jambo lolote," Lema alionya.

Pia aliwataka wagombea kutumia lugha ya staha na kutambua kwamba chama hicho ni cha wanachama wote.

"Wagombea watambue kwamba hawagombei dhidi ya mashetani, wanagombania nafasi dhidi ya wanachama wote, siasa za heshima si tu zinakijenga chama bali zinakifundisha chama tawala juu ya demokrasia tunayoishi...

"Minyukano, matusi na dhihaka kwenye mitandao itaonesha demokrasia tunayoihubiri tunashindwa kuiweka kwenye vitendo," Lema alionya zaidi.

Alisisitiza hisia na maoni ya wananchi juu ya kile kinachoendelea ndani ya chama hicho vinahitaji kujibiwa kwa tahadhari.

Lema pia alitoa tahadhari dhidi ya matumizi ya rushwa katika uchaguzi huo na kusisitiza yakemewe kwa vitendo.

Lema alisema: "Tunataka matumizi ya rushwa na fedha yakemewe kwa vitendo kuelekea katika uchaguzi wa ndani ya chama chetu, maana tunaposema rushwa ni adui wa haki, hatumaanishi chama tawala pekee, bali tunahusisha vyama vyote vya siasa kwa sababu ukipita kwa rushwa huwezi kuikemea."

Kumekuwa na mnyukano mkali katika mitandao ya kijamii miongoni mwa wafuasi wa Mbowe na Lissu baada ya viongozi hao kuingia katika kinyang'anyiro cha nafasi ya Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa.

Mara kwa mara Mbowe amenukuliwa na vyombo vya habari, likiwamo gazeti Nipashe, akiwataka wanachama na wafuasi wa CHADEMA kutoingia katika mtego wa wabaya wao kisiasa -- kutumia uchaguzi wa ndani kuharibu taswira ya chama hicho.

Lissu, kwa upande wake, amekuwa akijibu tuhuma mbalimbali zinazoelekezwa kwake na baadhi ya viongozi wa CHADEMA wanaoonekana kumuunga mkono Mbowe katika uchaguzi huo, baadhi akiwatuhumu waziwazi kutumiwa na baadhi ya viongozi wa serikali kuharibu ajenda za msingi za CHADEMA.

***Kwa maoni kuhusu habari hii na nyingine: +255 677 020 701 Email:customerrelations@guardian.co.tz***

# Saba wafariki ajali ya gari Handeni

**Na Mwandishi Wetu**

WATU saba wamefariki dunia jana na wengine 10 wakijeruhiwa katika ajali iliyohusisha gari aina ya lori na coaster katika Kijiji cha Michungwani wilayani Handeni, mkoani Tanga.

Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Albert Msando amethibitisha kutokea kwa ajali hiyo iliyotokea jana saa 12:00 asubuhi katika Barabara Kuu ya Segera na Chalinze.

Alisema kuwa chanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa dereva na kumwagiza Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Handeni (OCD) kuwachukulia hatua za kisheria madereva watakaokiuka sheria za usalama barabarani.

"Nimemwelekeza OCD atakayekiuka Sheria za Barabarani eneo la Handeni tutampandisha mahakamani na kuomba adhabu ya kifungo. Kwa ambao mmekuwa mkipiga simu kusaidiwa madereva wenu wakikiuka sheria za barabarani wala msisumbuke. Hakuna msaada zaidi ya kukaa lock up (jela) kwa mujibu wa sheria na kupandishwa kizimbani," alisema Msando.

"Ukifika Kijiji cha Manga Wilaya ya Handeni kwa dereva yeyote ambaye hatafuata sheria za usalama barabarani usitulaumu. Ajali nyingi zinaepukika. Na abiria, acheni kukaa kimya wakati dereva anaendesha ovyo, aidha shuka utarejeshewa nauli yako na toa taarifa kwa Jeshi la Polisi tudhibiti huu uzembe."

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Almachius Mchunguzi, alisema ajali hiyo imehusisha lori mali ya Kampuni ya Starling Gulf Trading likitokea Tanga kuelekea Dar es Salaam na basi dogo aina ya Toyota Coaster, mali ya Naman Joel Mkumbo, likitokea Dar es Salaam kuelekea Kilimanjaro.

Aliwataja majeruhi katika ajali hiyo ni dereva wa lori, Yohana Stephano (35), mkazi wa Goba, Dar es Salaam na utingo, Samweli Hossen (24), mkazi wa Dar es Salaam, Godlisen Minja (20) mfanyabiashara na mkazi wa Mabibo Dar es Salaam.

Wengine ni Loyce James (27) mkazi wa Buguruni Dar es Salaam, Lucy Urio (24) mkazi wa Dar es Salaam, Riziki Mboya (28) mkazi wa Njiapanda Moshi, Lina Swai (25) mfanyabiashara, Gospan Lema (24) fundi umeme na mkazi wa Temeke, Dar es Salaam.

Hivi karibuni kumekuwa na mfululizo wa matukio ya ajali za barabarani ambazo zimesababisha vifo vya Watanzania wengi.

Desemba 18 eneo la Mikese mkoani Morogoro gari aina ya coaster liligongana na lori la mizigo na kusababisha vifo vya watu 15.

Kadhalika, wiki iliyopita katika Kijiji cha Kabukome, Kata ya Nyarubungo wilayani Biharamulo basi la Kampuni ya Capro One lenye namba za usajili T857 DHW lilifeli breki katika mteremko na kurudi nyuma kisha kupinduka na kusababisha vifo vya watu 11 na wengine 16 kujeruhiwa.

Juzi, katika eneo la Same mkoani Kilimanjaro, aliyekuwa Mkurugenzi wa Utalawa na Usimamizi wa Rasilimaliwatu Ofisi ya Msajili wa Hazina, Amos Nnko, alifariki dunia kwa ajali ya gari.

***Kwa maoni kuhusu habari hii na nyingine: +255 677 020 701 Email:customerrelations@guardian.co.tz***

HABARI KITAIFA

## Bwana harusi anayedaiwa kujiteka kizimbani kwa mashtaka ya wizi

**Na Grace Gurisha**

BWANA harusi Vicent Massawe (36) anayedaiwa kujiteka, amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam na kusomewa mashtaka mawili, likiwamo la wizi wa gari alilopewa kwa ajili ya kutumia kwenye harusi yake.

Hata hivyo, Massawe amedai gari ambalo anatuhumiwa kuliiba namba T 642 EGU aina ya Toyota Ractis ni lake na nyaraka zote anazo na kuomba mahakama ihakikishe gari hilo linaletwa mahakamani kama dhamana yake.

"Gari hili lililotajwa kwamba nimeliiba si kweli, gari ni langu, lakini taarifa iliyotolewa na kusambaa inadai gari si langu. Ninaomba gari liletwe kama dhamana yangu hapa mahakamani," amedai Massawe.

Alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Beda Nyaki wa mahakama hiyo, akisisitiza atatimiza masharti ya dhamana kwa kuwa na mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni tisa ipo.

"Polisi walichelewa kunipa taarifa kuwa wananileta mahakamani, nikachelewa kutoa taarifa, lakini nimeshamwambia mke wangu yuko njiani anakuja hapa," alidai Massawe.

Hakimu Nyaki alimweleza mshtakiwa huyo kuwa ili awe nje kwa dhamana, anatakiwa awe na wadhamini wawili wenye vitambulisho vya taifa watakaotia saini bondi ya Sh. milioni tano na pia atatakiwa kuwasilisha mahakamani fedha taslimu au mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni tisa.

Mshtakiwa huyo hakutimiza masharti ya dhamana, hivyo alipelekwa mahabusu hadi Januari 7 mwakani kwa ajili ya kesi kutajwa na kuangalia hatua ya upelelezi ilipofikia kwa kuwa haujakamilika.

Kabla ya kuingia mahakamani, mshtakiwa huyo akiwa nje ya chumba cha mahakama, alionekana akicheka na kudai kuwa anashangaa polisi wameleta waandishi wa habari wengi kwa ajili yake.

"Haya pigeni picha, mkimaliza mtaniambia maana siwezi kujificha, ninashangaa hawa polisi wameniletea waandishi wa habari hivi," alidai.

Awali akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali Frank Rimoy alidai mshtakiwa anakabiliwa na mashtaka mawili aliyotenda akiwa ndani ya Jiji la Dar es Salaam.

Alidai Massawe ni mfanyabiashara na ni mkazi wa Kigamboni. Katika shtaka la kwanza, anatuhumiwa kuiba kama wakala. Inadaiwa Novemba 15 mwaka huu, akiwa eneo la Kigamboni ndani ya mkoa wa Dar es Salaam, aliiba gari hilo alilopewa na Silvester Beda kwa ajili ya kulitumia kwenye harusi yake.

Alidai kuwa gari hilo aliloazimwa, lilitakiwa kurudishwa lakini hakufanya hivyo. Thamani yake ni Sh. milioni 15 mali ya Beda.

Katika shtaka la pili, Massawe anadaiwa kuwa siku hiyo hiyo na eneo hilo, anatuhumiwa kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu Sh. milioni tatu kutoka kwa Beda, akiahidi kwamba angerudisha fedha hizo huku akijua si kweli.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, mshtakiwa huyo alikana kuhusika na tuhuma hizo.

Wakili Rimoy alidai upelelezi haujakamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa na kudai kuwa hawana pingamizi la dhamana kwa sababu mashtaka aliyoshtakiwa nayo yanadhaminika.

# Mwinyi ajivunia barabara mpya kupunguza msongamano, ajali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amewataka wananchi, kudumisha amani umoja na mshikamano ili kupata maendeleo.

Alitoa rai hiyo jana wakati akizungumza na wananchi katika uzinduzi wa barabara ya Uwanja wa Ndege - Mnazimmoja yenye urefu wa kilomita 6.5 iliyogharimu zaidi ya dola milioni tano.

Alisema ufunguzi wa barabara hiyo ni sehemu ya utekelezaji mradi wa ujenzi wa kilomita 100.9 za barabara za mjini ambazo zilikuwa katika hali mbaya na kujenga barabara za juu ili kupunguza msongamano.

Alisema lazima wahakikishe usafiri unakuwa mzuri katika mji wa Zanzibar kwa kuwa barabara za kisiwa hicho ni finyu na kuwafidia wananchi huwa ni gharama kubwa na ndio maana wameamua kujenga barabara zenye njia mbili.

Rais Dk. Mwinyi alisema kuwa baada ya kukamilika kwa ujenzi huo, hakuna nyumba zitakazoingiliwa na maji baada ya kujengewa miundombinu mingine ikiwamo mitaro pembezoni mwa barabara.

Alizungumzia pia matunzo ya barabara hizo, akiwataka madereva kuacha kuegesha gari katika njia za kupita watu kwa miguu.

Alisema kumeanza tabia za ovyo kuweka kifusi na kugeuza maegesho katika njia za watu kupita kwa miguu pembezoni mwa barabara na kutaka mfuko wa barabara kuhakikisha barabara hizo zinakuwa safi muda wote.

Dk. Mwinyi alisema barabara za juu anazojenga zinalenga kutengeneza mazingira mazuri ya barabara na kuwataka wananchi kuacha kujenga pembezoni mwa hifadhi za barabara.

Alisema wanapotaka kujenga barabara, gharama za fidia zinakuwa kubwa kuliko gharama ya ujenzi wa barabara, hivyo watu waache kujenga kwenye hifadhi za barabara na hifadhi hizo kutunzwa.

"Lazima mji uwe safi, hivyo tutafanya programu maalumu kuhakikisha barabara mpya zote zinakuwa na taa ili ziendane na mazingira," alisema.



Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Muhammed alisema wameshakamilisha ujenzi wa barabara za kilomita 86, zikiwamo barabara za ndani.

Alisema ujenzi wa barabara zingine unaendelea vizuri na utakamilika kwa wakati (Novemba mwakani). Alisema mafanikio hayo yanatokana na miomgozo na maono ya Rais Dk. Mwinyi anayotoa kwa wizara hiyo.

Alisema wakati barabara hiyo inajengwa kulikuwa na maneno mengi ya kejeli, kwamba barabara haihitaji kujengwa upya ilhali ilijengwa miaka ya 70 na haikuwa inakidhi viwango vya kisasa.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Habiba Hassan Omar, alisema barabara hiyo ni miongoni mwa barabara zenye urefu wa kilomita 100.9 zinazojengwa kisiwani.

Mkuu wa Mkoa Idrisa Kitwana Mustafa alisema barabara hiyo itapunguza ajali na vifo vitokanavyo na ajali za barabarani kisiwani Zanzibar.

*Kwa maoni kuhusu habari hii na nyingine: +255 677 020 701 Email:customerrelations@guardian.co.tz*

# NEMC yaunda timu kudhibiti kelele kwenye kumbi za starehe Krismasi

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limeunda timu ya operesheni maalumu ya kufuatilia na kuwachukulia hatua za kisheria wachafuzi wa mazingira na kelele kwenye kumbi za starehe wakati wa sikukuu.

Hayo yalisemwa jana Dar es Salaam na Kaimu Mkurugenzi wa Utekelezaji Sheria wa baraza hilo, Jamal Baruti wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye ofisi za baraza hilo zilizoko Mikocheni.

Alisema timu hiyo itafanya kazi kwa kanda zote za baraza nchini katika msimu huu wa sikukuu. Kwa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kutakuwa na timu ambazo zitakuwa zinatembelea maeneo yote yatakayotolewa taarifa kuwa na changamoto za kimazingira na kufanya utatuzi kwa mujibu wa sheria na kanuni husika.

Baruti alisema katika kuhakikisha zoezi hilo linakuwa na ufanisi mkubwa, baraza limejipanga kutekeleza zoezi hilo kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa husika, wananchi na mamlaka zingine za serikali, likiwamo Jeshi la Polisi.

"Baraza limejipanga kupokea na kufanyia kazi taarifa zote zinazohusiana na uvunjifu wa sheria ya mazingira kutoka kwa wananchi wema. Baraza kupitia timu yake maalumu ya upokeaji taarifa (Call Centre Team) litakuwa linapokea taarifa mbalimbali juu ya matukio ya uvunjifu wa Sheria ya Mazingira kwa muda wa saa 24.

"Baraza linatoa rai kwa taasisi, kampuni na watu wote nchini kuhakikisha wanaendelea kuzingatia sheria ipasavyo bila shuruti kwani uchafuzi wa mazingira wa sauti na mitetemo iliyozidi viwango na utiririshaji maji taka ni hatari kwa afya ya binadamu.

"Sambamba na hayo, inashauriwa kufuata taratibu za kisheria katika kupata vibali kutoka katika mamlaka husika kabla ya kufanya mikusanyiko ya sherehe," alisema.

Baruti alisema baraza limejikita zaidi katika kuendelea kutoa hamasa na elimu kuhusiana na uzingatiaji Sheria ya Mazingira kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

"Kwa wale wote ambao watabainika kukaidi uzingatiaji Sheria ya Mazingira na kanuni zake, hatua stahiki za kiutawala na kisheria zitachukuliwa," alisisitiza.

Alisema kuwa miaka kadhaa iliyopita katika kipindi kama hiki cha msimu wa sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya, NEMC ilibaini kuongezeka kwa matukio ya uchafuzi wa mazingira kwa njia ya sauti na mitetemo iliyozidi viwango pamoja na utiririsha maji taka toka viwandani.

Alisema uchafuzi wa mazingira wa namna hiyo umekuwa unatokea katika miji mikubwa ambayo ina idadi kubwa ya watu na ongezeko kubwa la shughuli za kiuchumi kama vile Dar es Salaam, Pwani, Arusha, Mwanza, Mbeya na maeneo mengine ya mikoa ambayo inakua kiuchumi kwa kasi.

Kaimu Mkurugenzi huyo alisema kuongezeka kwa sauti na mitetemo inayozidi viwango vya kisheria hutokea katika maeneo ya mikusanyiko ya watu na maeneo ya starehe kama vile maeneo ya vilabu (baa), kumbi za starehe na maeneo mengine ya mikusanyiko ya watu katika jamii.

Nipashe WhatsApp Chaneli

Skani hapa kutembelea chaneli yetu

# Serikali yaita sekta binafsi kuwekeza katika usafiri wa waya, mabasi mwendokasi, reli

**Na Elizabeth Zaya**

WIZARA ya Uchukuzi kwa kushirikiana na taasisi zake ikiwamo Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imealika sekta binafsi kuwekeza katika huduma ya usafirishaji wa reli, usafiri wa waya na usafirishaji maalumu kwenye majiji makubwa kupitia barabara.

Kwa mujibu wa wizara hiyo, miongoni mwa maeneo wanayotaka sekta binafsi iwekeze ni pamoja na usafiri wa mabasi yaendayo kasi katika majiji.

Wakizungumza kwenye mkutano wa kujadili kanuni za usafirishaji, viongozi kutoka wizara hiyo walisema kanuni hizo zimetokana na maendeleo ambayo serikali imeyafanya hasa kwenye ujenzi wa reli na barabara.

Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Barabara kutoka wizara hiyo, Henry Magombana, alisema wamefanya mapitio ya kanuni hizo kutokana na maboresho ya sheria za sasa za usafirishaji.

"Leo wizara imeita wadau kwa ajili ya kupitia kanuni kuu tatu ambazo zimetokana na maendeleo ambayo serikali imeyafanya kupitia miradi mikubwa.

"Na miongoni mwa kanuni hizo ni pamoja na ile inayohusu huduma za usafiri wa waya ambayo tutaanza kusajili na kuwadhibiti watoa huduma wa usafiri huu, pia tunawakaribisha watoa huduma binafsi kwenye huduma ya usafiri wa reli, barabara na usafiri maalumu wa barabara katika majiji na hii itakuwa inatolewa leseni maalumu," alisema.

Aliongeza kuwa usafiri huo katika majiji unawezesha wadau kutoa huduma, akitolea mfano Jiji la Dar es Salaam na majiji mengine yote yanakaribishwa wawekezaji ambao watatakiwa kuomba leseni baada ya kanuni kutoka.

Alisema sababu za kuboresha kanuni hizo zinajumuisha kuruhusu sekta binafsi kutoa huduma katika maeneo tajwa.

Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo, alisema leseni maalumu ambayo itatolewa kwa watoa huduma maalumu kwenye barabara katika majiji, inalenga zaidi usafiri wa mabasi ya mwendoksi.

"Kwahiyo serikali inataka watu binafsi ndio watoe huduma, inaweza kuwa watu wenye mabasi yao hapa mjini wakajiunga wakapewa mkataba wa kuendesha lakini nauli yao itakuwa maalumu, kwa sababu hata njia nayo ni maalumu.

"Kikubwa hapa tunajaribu kuangalia utaratibu ambao tutatoa leseni kwa mabasi ya mjini na maeneo ya miji kwenda nje kidogo na si kutoka Dar es Salaam kwenda mikoani, tunafanya hivyo kwa sababu tuna tatizo kwenye usafiri wa mjini," alisema.

Kuhusu usafiri wa waya, Suluo alisema unalenga zaidi kukuza shughuli za kitalii na kwamba katika sehemu zote ambazo walipita na kufanya utafiti, watu wengi wanaotumia usafiri huo wa waya ni kwa ajili ya kitalii.

"Na kanuni hii inakwenda kuangalia usalama wa kuwekeza, miundombinu yake pamoja na uendeshaji," alisema Suluo.



Waandishi wa habari mkoani Shinyanga wakitembelea maendeleo ya ujenzi wa uwanja wa ndege uliopo Ibadakuli Manispaa ya Shinyanga juzi, ambao kwa sasa umefikia asilimia 80 na unatarajiwa kukamilika Aprili mwakani kwa gharama za Sh. bilioni 44.8. **PICHA: MARCO MADUHU**

MAAFA YA MVUA SAME:

# Mamia washiriki mazishi ya mume na mke

**Na Idda Mushi,** SAME

MAMIA ya wananchi wa Same wamejitokeza katika kijiji cha Mjema, kata ya Bombo, wilayani Same, mkoa wa Kilimanjaro kuaga miili ya mume na mke ambao ni miongoni mwa watu sita waliopoteza maisha baada ya nyumba walizokuwa wanaishi kuangukiwa na kifusi.

Vifo vya watu hao viliripotiwa juzi, chanzo kikiwa ni mvua kubwa inayoendelea kunyesha maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Kasilda Mgeni aliwaongoza wananchi hao katika maombolezo hayo na kushiriki ibada ya kuaga mwili wa marehemu Eliakunda Mrutu katika kijiji cha Duma, kata ya Msindo ambaye naye nyumba yake iliangukiwa na kifusi na akapoteza maisha katika mkasa huo wa mvua iliyonyesha kwa siku tatu mfululizo wilayani humo.

Kasilda mbali na kutoa pole kwa waombolezaji, ndugu, jamaa na marafiki waliowapoteza ndugu zao katika tukio hilo, alisema uharibifu wa mazingira unaotokana na shughuli za kibinadamu ndio uliochangia kwa kiasi kikubwa milima kuporomoka na kusababisha madhara, vikiwamo vifo, uharibifu wa mazao na miundombinu ya barabara.

Aliwasisitiza wananchi wa wilaya hiyo kuchukua tahadhari kwa kuhama kwa muda katika maeneo hatarishi ili kuepuka madhara zaidi yanayoweza kuendelea kujitokeza wakati huu mvua inapoendelea kunyesha.

Pia aliwataka wananchi walio kwenye maeneo yaliyokumbwa na maafa kuwa watulivu katika kipindi hiki wakati serikali inaendelea na tathmini ya athari ya mafuriko na kuendelea na mipango mbalimbali ya kurudisha miundombinu yote iliyoharibiwa na mvua.

"Baadhi ya watu wamejenga hadi kwenye vilele vya milima, hii ni hatari sana. Mwenyezi Mungu alikuwa na maana yake kuweka miti ambayo imeshikana na udongo, mawe na majani.

"Sasa unapotoa kimoja kwa shughuli za kilimo ama sababu zingine, unafanya vinashindwa kuhimili na kusababisha madhara kama haya, lazima tuchukue hatua kwa kurejesha uoto huu wa asili ulioharibiwa kwa kupanda miti kudhibiti madhara zaidi," alisema.

Baadhi ya waombolezaji kutoka kijiji cha Mjema, akiwamo Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Jeremiah Mjema na Beatrice Mjema walisema matukio ya kuporomoka kwa milima kwenye maeneo yao yamekuwa yakijirudia mara kwa mara hasa nyakati za mvua kubwa inaponyesha hali ambayo si ya kawaida kwao.

Taarifa ya Kamati ya Maafa ya Wilaya ya Same imeonesha maeneo yaliyoathiriwa zaidi na mvua hiyo ni pamoja na kata za Msindo, Vuje, Bombo, Mtii na Maore.

Mbali na vifo vya watu sita, nyumba 25 zimeangushwa na maji huku kukishuhudiwa uharibifu wa miundombinu, ikiwamo barabara hasa maeneo ya milimani ambayo hivi sasa hayafikiki kwa urahisi.

## Polisi yakamata mabasi manne yaliyozidisha abiria

**Na Benny Kingson,** TABORA

JESHI la Polisi Mkoa wa Tabora limekamata mabasi manne yanayodaiwa kuzidisha abiria katika doria zake za kipindi hiki cha msimu wa sikukuu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Richard Abwao, akitoa taarifa kwa waandishi wa habari jana ofisini kwake, alisema wanaendelea kufanya operesheni kabambe kuwasaka wahalifu na wavunjaji sheria.

Alisema kuwa katika kipindi hiki cha msimu wa sikukuu, kuna ongezeko la watu kuingia na kutoka katika mkoa huo, hivyo wanaendesha doria katika maeneo mbalimbali kuwasaka wahalifu na kufanya mkoa kuendelea kuwa salama.

"Tunafanya doria kwa kutumia askari wetu wenye magari, mbwa na wa miguu na tumefanikiwa kukamata mabasi manne yaliyozidisha abiria.

"Kitendo hiki ni cha uvunjifu wa sheria na kinahatarisha usalama wa abiria na mali zao, hivyo tutaendelea kufuatilia magari yote katika kipindi hiki na wakati wote," alisema.

Kamanda huyo alisema ametoa maelekezo kwa askari wa kata zote kusimamia vikundi vya ulinzi shirikishi ili kulinda amani na usalama wa watu katika maeneo yao, akisisitiza kuwa wamejipanga kutoa ulinzi wa kutosha katika nyumba za ibada na makazi hasa kipindi hiki cha sikukuu.

Aliwata watakaohitaji kupiga fataki kwenda kuchukua vibali na maelekezo ya jinsi ya kupiga, akiwaonya wenye tabia za kuchoma vitu barabarani na kufanya fujo na uharibifu kwamba watakamatwa.

Kamanda huyo pia aliwahimiza madereva kutotumia vilevi wakiwa wanaendesha magari wakati wote na kuzingatia sheria za usalama barabarani.

"Wamiliki wa kumbi za starehe wachukue tahadhari kwa kuhakikisha kunakuwa na hewa ya kutosha, kuchukua watu kwa idadi isiyozidi uwezo wao na kuwa makini kwa wote kwa kuwafuatilia watoto wote waliomo ndani ya kumbi na muda wa kumaliza na kutoka ni saa 12:00 jioni ili wawahi majumbani," aliagiza.

## HABARI KITAIFA

# Mbaroni kwa tuhuma za mauaji, wizi wa bodaboda

**Na Said Hamdani,** LINDI

JESHI la Polisi mkoani Lindi linamshikilia mkazi wa kijiji cha Mtumbya, kata na Halmashauri ya Mtama, Hassani Omari (30) kwa tuhuma za mauaji na wizi wa mali.

Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) John Imori alitoa taarifa hiyo jana alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari kuhusu masuala mbalimbali.

Alisema mtuhumiwa huyo anadaiwa kufanya tukio la mauaji na wizi Desemba 10 mwaka huu, saa mbili usiku baada ya kumkodi dereva pikipiki Azizi Omari (28) kwa lengo la kumpeleka sehemu alikotaka.

Kamanda Imori alisema kuwa tangu bodaboda huyo akodiwe na mtuhumiwa, hakuonekana tena katika maeneo alikokuwa anafanyia biashara yake.

Alisimulia kuwa Desemba 22, mwaka huu, saa 11 jioni, mwili wa kijana huyo uliokotwa porini katika kijiji cha Mtumbya, jambo lililothibitisha kuwa aliuawa.

"Huyu bodaboda alikodiwa na mtuhumiwa ili ampeleke safari yake, lakini kuanzia hapo hakurejea hadi mwili wake ulipokutwa porini," alisema Kamanda Imori.

Alisema mtuhumiwa alikamatwa katika kijiji cha Mkunya, wilayani Newala, mkoani Mtwara akiwa anaendesha pikipiki ya marehemu yenye namba za usajili MC 559 EAL.

Kamanda Imori alisema mtuhumiwa amesharejeshwa mkoani Lindi na atafikishwa mahakamani muda wowote kuanzia ili kujibu mashtaka yanayomkabili baada ya upelelezi kukamilika.

Kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni za Adhabu, SURA 16, ikiwa mtuhumiwa huyo akipatikana na hatia mahakamani, adhabu ya kosa la kuua kwa kukusudia ni kunyongwa hadi kufa.



Brigedia Jenerali George Itang'are (kushoto), akipokea zawadi kutoka kwa Luteni Kanali Joseph Mushilu (kulia), ambaye ni kamanda wa kundi la saba la walinda amani wa Tanzania katika Ujumbe wa Umoja wa Mataifa nchini Jamhuri ya Afrika ya Kati, ambaye alikamilisha jukumu lake. Sherehe ya kuwapokea ilifanyika Chuo cha Mafunzo cha Kijeshi Mapinga wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani juzi. **PICHA: JESHI LA WANANCHI**


## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MOHAMEDI NASSORO PAURI**

Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 903 DVR,** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu nayeye.

**PHQ/MOR/MOR/44863/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TEMEKA**

**Kituo cha Jumuishi Mkoa DAR ES SALAAM**

**USIMAMIZI WA MIRATHI NO. 2858/2024**

**Katika shauri la mirathi ya marehemu ASIA ISSA MFAUME wa KIGAMBONI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA FATUMA ALLY MFAUME**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 52 ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama ya Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/ maslahi yoyote ya mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaharifiwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mapema tarehe 21 Mwezi 01 mwaka 2025 kabla huyo muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia**

Endapo kama yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuleta mahakamani kukaguliwa.

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

Imetolewa leo tarehe 24 mwezi 12 mwaka 2024

HAKIMU

## KUPOTEA KWA CHETI



**JAPHET JIRORI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index No. **S.110-0046** Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ILBORU SECONDARY SCHOOL** mwaka 2001, Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **CONTROL NUMBER 9910843282139**



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni muhimu kupambana na mabadiliko tabianchi

**UCHAFUZI** wa mazingira umeleta athari kubwa katika mabadiliko ya tabianchi, hali iliyosababisha baadhi ya maeneo kukosa mvua na kuleta upungufu wa mvua.

Athari za mabadiliko ya tabianchi zimeshuhudiwa katika baadhi ya maeneo ambako mvua imenyesha kupita kiwango na watu kukosa makazi na hata kusababisha vifo.

Umuhimu wa kuhifadhi mazingira unatakiwa uanzie katika ngazi ya familia na kupanua wigo hadi kwa wadau mbalimbali.

Watu muhimu na wanaosikilizwa katika jamii ni viongozi wa dini ambao Waziri Mkuu Kassim Majaliwa aliwahi kusema kuwa wanayo nafasi kubwa na kuwataka iwe ajenda maalum katika ofisi za umma, za binafsi au kwenye taasisi.

Umuhimu wa jamii kushiriki katika uhifadhi mazingira ni kuunga mkono juhudi za Rais Dk. Samia Suluhu Hassan za kuendelea kuimarisha uhifadhi na usimamizi wa mazingira nchini.

Aidha, jitihada ambazo Rais Samia amezichukua ili kuhakikisha suala la nishati safi linakubalika ni kukataa kukata miti na kuhamasisha kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Rais Samia amekuwa kinara wa nishati na alienda nchini Ufaransa kuhutubia kuhusu nishati safi na yeye akiwa ni Mwenyekiti mwenza wa mkutano huo, jambo ambalo ni ni fahari kwa nchi ya Tanzania.

Wajasiriamali wamepewa fursa kuanzisha biashara ya kuuza mitungi na majiko ya gesi hadi kwenye ngazi ya vijiji ili nishati hiyo iweze kupatikana kwa urahisi hali ambayo itaweka ukomo wa matumizi ya mkaa na kuni nchini.

Pia, serikali imechukua hatua za kisera na kimkakati ili kuleta matokeo chanya zikiwamo za kuandaliwa kwa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021; Kutungwa kwa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2014; kuandaa na kutekeleza Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira wa mwaka 2022 hadi 2032; kuandaa na kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 2021 hadi 2026; na kutungwa kwa Kanuni na Miongozo inayohusu masuala ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi.

Wizara inayosimamia mazingira imetakiwa ishirikiane kwa karibu na wizara za kisekta kuhakikisha maadhimisho mbalimbali ya kitaifa yanayogusa masuala ya mazingira yanatumika kikamilifu kuwezesha jamii kupata uelewa na kuweka alama za kudumu na matokeo yanayopimika kuhusu utunzaji mazingira ikiwamo Siku ya Upandaji Miti, Siku ya Hali ya Hewa, Siku ya Maji, Siku ya Ardhi Oevu, Siku ya Mazingira na Siku ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni.

Uhamasishaji kuhusu utunzaji wa mazingira, Waziri Mkuu ameziitaka ofisi za mikoa na wilaya, zisimamie suala hilo na kusisitiza kuhusu umuhimu wa kuzingatia sheria na kanuni za mazingira na ikibidi watumie mitandao ya kijamii kusambaza elimu hiyo.

Hiyo itasaidia kuongezeka kwa ufahamu miongoni mwa jamii kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa mazingira na kutasaidia kupunguza uharibifu na kuimarisha usimamizi wa mazingira. Aidha, elimu ijumuishe matumizi endelevu ya rasilimali za mazingira ikiwamo matumizi bora ya ardhi, maji na nishati ili kuhakikisha kuwa rasilimali hizo zinabaki kuwa za kudumu kwa vizazi vijavyo.

Utunzaji wa mazingira unaanzia nyumbani kwako, sehemu yako unayofanyia shughuli za kukuingizia kipato na hata barabarani unapopita.

Kila mmoja anapoona mwenzake akiharibu mazingira ana jukumu la kumkemea ili ajue kuwa anachokifanya kinaathiri jamii na taifa kwa ujumla.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Vijana sikukuu kuweni makini

**HERI** ya Noeli vijana. Imekuwa ni kawaida kwa baadhi yenu hasa wakazi wa mijini kuchangishana fedha na kukodi magari kwenda ufukweni kusherehekea sikukuu.

Mkiwa huko mnaogelea na kufanya mambo mengine ya burudani pamoja na matendo yanayokiuka maadili.

Katika safari zenu za kwenda 'beach' au ufukweni, mwendo ambao dereva huendesha, si wa usalama bila kujali kuwa wapo wengine wanaoning'inia madirishani na wengine milangoni.

Mkiwa katika mazingira hayo, mnajisahau mnashangilia na kupiga kelele kumhimiza dereva kuongeza mwendo.

Ili kukoleza mukari wapo wanaogonga gari na kupuliza mavuvuzela kwa raha zao kana kwamba wanachokifanya ni sahihi.

Vijana hao wanapokuwa katika safari hiyo wana vinywaji vikali ndani ya gari, wengine wameshakunywa kitendo kinachoashiria kuwa wanakwenda kulewa na licha ya kwamba wengine walianza kulewa kabla ya safari.

Leo ni Sikukuu ya Krismasi, ninaomba niwakumbushe vijana wenye mtindo huo kuwa ni vyema washerehekee kwa umakini, wasiruhusu kujiweka katika mazingira hatarishi kama ambavyo wamezoea kufanya.

Si vibaya kukodi gari kwenda beach, lakini ni vibaya kukodi gari na kumtaka dereva aendeshe mwendo ambao si salama kwao na pia si salama kwenda huko na kufanya vitendo visivyofaa ukiwamo vya ngono.

Ninaamini kwamba mtu anapozidiwa na pombe, anaweza kufanya vitendo visivyofaa, hivyo, hata madereva wanaokodishwa kwenda kusherehekea sikukuu wakilewa, ni hatari zaidi kwa hao waliokodisha gari.

Watahoji kwa nini sababu ni kwamba umakini wawapo barabarani unapotea na kujikuta wakisababisha ajali ambazo wakati mwingine zingeweza kuzuilika iwapo wangekuwa makini kwa kuepuka kunywa vilezi na kuendesha magari.

Vilevile madereva wa bodaboda nao hawako nyuma. Kila siku baadhi yao hukesha wakilewa kwa mtindo ambao wanauitwa 'kutoa loki'. Hao nao wakati wa sikukuu huwa wanalewa pombe zaidi hasa 'viroba.'

Sio kwamba wanalewa na kurudi nyumbani, bali huingia barabarani kubeba abiria, tena wakati mwingine zaidi ya mmoja (mishkaki) bila kujali kwamba wanaiweza na kujikuta wakiwabwaga.

Kitendo hicho kinaweza kusababisha wenyewe na abiria wao kupoteza maisha au kupata ulemavu wa kudumu na hivyo kujikuta wakiwa tegemezi kwa familia au kwa ndugu na jamaa.

Ninadhani kwa wakati huu wa sikukuu ipo haja kwa vyombo vya dora kuongeza mikakati ya kukabiliana na watu wa aina hiyo ili kuokoa maisha yao badala ya kuwaacha wakisherehekea wanavyotaka.

Biashara ya bodaboda inagharimu maisha ya watu kutokana na uzembe wa baadhi ya madereva wake kwa kutozingatia maelekezo wanayopewa ili waweze kuwa salama wakati wote wanapoendesha vyombo hivyo.

Wengi wa madereva wa bodaboda ni vijana ambao wanategemewa kuwa taifa la sasa na la kesho, lakini inasikitisha kuona baadhi yao wakijihusisha na ulevi huku wakiendesha vyombo vya moto.

Sheria ziko wazi kwamba mtu hawezi kuendesha chombo cha moto akiwa amelewa, hiyo ni kwa ajili ya usalama wake na wale aliowabeba, lakini ajabu ni kwamba vijana wa bodaboda hawazingatii hilo.

Pamoja na katazo hilo, imekuwa ni kawaida kwao kulewa siku zote. Kwa hali kama hiyo, ni wazi kwamba wakati wa sikukuu wanaweza kujiachia zaidi bila kujali usalama wao na hata wa abiria wao.

Mazingira hayo ndio yanayonisukuma kuwashauri wawe makini kwamba kuna maisha baada ya sikukuu, hivyo, uhai ni muhimu kuliko sikukuu ambazo huzichukuliwa kuwa ni za kulewa kupita kiasi.

Niwatakie sikukuu njema yenye amani na utulivu itakayoisha bila kuwapo ajali za kizembe zinazotokana na ulevi wa kupindukia ambao unagharimu maisha ya watu na kuangamiza nguvu kazi ya taifa.

HABARI KITAIFA

# Waziri awataka wananchi kulinda samaki kukuza uwekezaji, uchumi

**Na Thobias Mwanakatwe**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Dk. Ashatu Kijaji, amewataka wananchi wanaojihusisha na shughuli za uvuvi wa samaki kulinda rasilimali hizo ili wawekezaji waliowekeza viwanda vya kuchakata samaki wapate malighafi za kutosha.

Alitoa rai hiyo juzi baada ya kutembelea kiwanda cha kuchakata samaki cha Pride of Nile PVT Ltd kilichoko wilaya ya Muleba, mkoani Kagera.

Dk. Ashatu alisema ili uwekezaji huo uwe na matunda yanayotokana na juhudi za serikali za kuimarisha mazingira bora na wezeshi sambamba na kuhamasisha sekta binafsi, kuna umuhimu kulinda rasilimali za samaki na hivyo kupanua wigo wa kuongeza thamani ya mazao ghafi ya sekta za uzalishaji, ikiwamo uvuvi.

"Jukumu letu kama watanzania kwa sasa ni kuzilinda rasilimali hizi za asili kwa wivu mkubwa kwa sababu mbali na kutupatia ajira na kipato kwa mtu mmoja mmoja, rasilimali hizi pia zinanufaisha uchumi wa nchi kwa ujumla," alisema.

Dk. Ashatu pia alitoa rai kwa wananchi kuongeza nguvu kwenye ufugaji samaki kwa njia ya vizimba ili kupumzisha shughuli za uvuvi wa asili na kuwapatia nafasi samaki wa asili (wild fish) kuzaliana kwa wingi.

"Ninakuagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuongeza kasi ya uhamasishaji ufugaji samaki kwa vizimba," alielekeza.

Mkuu wa Wilaya ya Muleba, Dk. Abel Nyamahanga, alisema asilimia 70 ya eneo la wilaya hiyo limezungukwa na maji ya Ziwa Victoria na hivyo kufanya sehemu kubwa ya wakazi wake kuwa wavuvi, jambo linalowafanya kuwa na kila sababu ya kulinda rasilimali za ziwa hilo kwa nguvu kubwa.

Awali akisoma taarifa ya mchango wa kiwanda chao kwenye soko la ajira, Meneja Ubora wa kiwanda hicho, Hamza Mustapha alisema kimeajiri watanzania 125 na wanachangia uchumi wa taifa kwa kulipa mrabaha na kodi mbalimbali za serikali.

Hamza alisema upatikanaji mdogo wa malighafi hususani samaki aina ya sangara unasababisha kiwanda hicho kutumia chini ya asilimia 50 ya uwezo wake uliosimikwa.

"Tunaomba serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ije na mkakati shirikishi wa kuhakikisha kunapatikana sangara wa kutosha kwa ajili ya kulisha viwanda ili kukuza mauzo nje na kulingizia taifa fedha za kigeni," alisema.

Dk. Kijaji baada ya kuapishwa, amekuwa ziara katika mikoa ya Kanda ya Ziwa. Tayari ameifikia mikoa ya Mara, Mwanza na Kagera, akilenga kufuatilia ufanisi wa sekta, kusikiliza na kupokea changamoto na mapendekezo ya wadau.




Aliyekuwa Spika wa Bunge la Wananchi kupitia CHADEMA, Celestine Simba, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu nia yake ya kugombea nafasi ya uenyekiti wa Baraza la Wanawake - BAWACHA. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Othman: Ujenzi nyumba za watumishi utaboresha huduma za matibabu Z'bar

**Na Mwandishi Wetu,**
PEMBA

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kuimarisha huduma za afya, ikiwamo kujenga nyumba za wafanyakazi.

Othman ambaye ni Mwenyekiti wa Taifa wa ACT- Wazalendo alisema hayo katika Hospitali ya Wilaya ya Wete iliyoko Kinyasini, Mkoa wa Kaskazini Pemba alipozungumza na wananchi baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa nyumba za wafanyakazi wa hospitali hiyo ikiwa ni shamrashamra za sherehe za miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Makamu wa Rais alisema hatua hiyo ya serikali pia inakwenda sambamba na uwekaji vifaa vya kisasa vya huduma za afya ili kuwapatia wananchi wa Zanzibar huduma bora za afya na kuhakikisha upatikanaji huduma za matibabu ya dharura.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inafarajika kuona inaendelea kusimamia na kuhakikisha watoa huduma za afya wanapatiwa makazi bora ili watoe huduma bora kwa wananchi na kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yao.

Othman alisema ujenzi wa makazi ya watumishi karibu na hospitali na vituo vya afya utawasaidia watumishi kupunguzia gharama za usafiri na kusafiri umbali mrefu.

Alielekeza uongozi wa Wizara ya Afya kuanza kufikiria namna bora na utaratibu sahihi wa kutunza nyumba hizo kwa kuzingatia kuwapo mpango wa kuzikarabati kwa wakati.

Makamu wa Rais aliwaomba wananchi hasa wa wilaya hiyo na maeneo jirani kuendelea kutoa ushirikiano kwa kuitumia hospitali hiyo ipasavyo kufanya uchunguzi wa maradhi kwa kufuata utaratibu wa rufani za matibabu kwa mujibu wa miongozo ya Wizara ya Afya.

Othman pia alitoa rai kwa wananchi kujitahidi kujikinga dhidi ya maradhi mbalimbali kwa kuwa kinga ni bora kuliko tiba na kufanya hivyo kutapunguzia serikali mzigo wa gharama za kuwatibu wananchi wanaopata ugonjwa ambao ungeweza kuepukika.

Makamu wa Rais pia alielekeza uongozi wa mkoa wa Kaskazini Pemba kushirikiana na Wizara ya Afya kuhakikisha kipande cha barabara inayoingia hospitalini huko kutoka eneo la barabara kuu ya Kinyasini hadi hospitalini, inajengwa ili kuondoa usumbufu kwa wagonjwa hasa wajawazito.

Nyumba hizo zinazojengwa zinatarajiwa kuchukua familia 16 za watumishi, zikitarajiwa kuongeza tija kwa madaktari na wafanyakazi wengine katika kuimarisha upatikanaji huduma bora kwa wananchi.

Akimkaribisha Makamu wa Rais, Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui alisema dhamira ya wizara hiyo ni kuhakikisha upatikanaji huduma bora za afya kwa wananchi na pia kupunguza vifo vya mama na mtoto kwa kutengeneza mazingira mazuri ya utoaji huduma kwa umma.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk Khatib, alisema ujenzi wa nyumba hizo ni sehemu ya kuendeleza miradi ya maendeleo kutimiza lengo la mapinduzi.


Alisema kwa mwaka huu miradi 16 itawekwa mawe ya msingi, kuzinduliwa na mingine kufunguliwa ndani ya mkoa huo.

Akitoa taarifa ya kitaalamu, Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Zanzibar, Miraji Mzee Mgereza alisema mradi huo hadi utakapokamilika utagharimu Sh. bilioni 4.1 na utaondoa usumbufu kwa madaktari na wafanyakazi wengine katika hospitali hiyo.

Kilele cha sherehe za kutimiza miaka 61 tangu Mapinduzi ya Januari 1964 zinatarajiwa kufanyika kisiwani Pemba Januari 12 mwakani. Hivi sasa serikali iko kwenye uzinduzi na uwekaji mawe ya msingi kwa miradi mbalimbali ya maendeleo.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Polisi yatahadharisha abiria kuepuka kula ovyo

**Na Steven William,** MUHEZA

JESHI la Polisi Wilaya ya Muheza, limetoa tahadhari kwa abiria wanaosafiri kwenda mikoani kipindi cha Sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya wanaotumia mabasi kuwa waangalifu na matapeli.

Wito huo ulitolewa juzi na Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya ya Muheza, Leonard Bandola, wakati akitoa elimu kwa abiria katika mabasi yanayosafiri kwenda mikoani katika stendi kuu wilayani hapa.

Alisema, kipindi cha kuelekea Sikukuu ya Krismasi na mwaka mpya kumekuwa na matukio mbalimbali ikiwamo watu kutapeliwa fedha na mizigo katika mabasi.

Bandola alisema, abiria wanaopanda katika mabasi wasikubali kushirikiana na abiria mwingine kula chakula chochote hata tunda kwa kuwa wengine wanaweka dawa za kulevya ili kuwaibia abiria wakisisinzia ndani ya basi.

Katika hatua nyingine kamanda huyo aliwaasa abiria kutoa taarifa kwa polisi kutumia namba za polisi zilizopo katika mabasi hayo wakiona dereva anakwenda mwendo kasi ama kufanya uzembe wowote barabarani ikiwamo kuyapita magari mengine kwenye kona ama dereva kulewa.

Bandola alisema kuwa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, limejipanga kudhibiti madereva kwenda mwendo kasi, walevi na wanaofanya makosa mbalimbali ya usalama barabarani.

Alisema pia jeshi hilo limejipanga kufanya doria za miguu, magari na pikipiki katika kipindi hiki cha sikukuu ili kudhibiti uhalifu na wakristo washerehekee sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya kwa amani na utulivu wakiwa katika starehe, majumbani na nyumba za ibada.



Mbunge wa Ndanda, Cecil Mwambe, akikabidhi mitungi 160 ya gesi kwa viongozi wa Jumuiya za CCM ikiwa ni sehemu ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia katika hafla iliyofanyika mjini Masasi jana. **PICHA: HAMISI NASRI**

# Mbunge atoa msaada mitungi 160 gesi ya kupikia

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MBUNGE wa Jimbo la Ndanda (CCM), Cecil Mwambe, ametoa mitungi 160 ya majiko ya gesi ya kilo sita kwa viongozi wa Jumuiya ya Umoja wa Wazazi, Wanawake (UWT) na Umoja wa Vijana (UVCCM) wa jimbo la hilo.

Lengo likiwa ni kuhamasisha jamii kujikita katika matumizi ya nishati safi.

Akiongea katika mafunzo ya itikadi na uongozi kwa viongozi hao Jumuiya za CCM kutoka kata za Jimbo la Ndanda, mafunzo ambayo yamefanyika katika ukumbi wa jengo la zamani la halmashauri ya wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, alisema lengo ni kuunga mkono ajenda ya serikali kupiga vita mabadiliko ya tabianchi na uchafuzi wa mazingira.

Alisema matumizi ya nishati safi ya kupikia yatasaidia kutunza mazingira na uchafu wa mazingira na viongozi hao kwa sasa hawapaswi kutumia mkaa na kuni kwa kutunza mazingira.

Mwambe alisema viongozi hao ni muhimu katika ngazi ya kata na yeye ataendelea kushirikiana vema na jumuiya hizo katika kuleta maendeleo katika Jimbo la Ndanda.

"Natumia fursa hii kumpongeza Rais Dk. Samia Suhulu Hassan kwa kutoa fedha nyingi za miradi ya maendeleo katika Jimbo la Ndanda na tutaungana naye katika kuhifadhi na kutunza mazingira," alisema Mwambe.

Pia viongozi hao wa Jumuiya za CCM wamepatiwa mafunzo ya itikadi na uongozi ili kuwajengea uwezo wa kiutendaji katika majukumu yao.

Aliwataka viongozi hao kuendelea kushikamana pamoja ili kudumisha umoja ndani ya chama ili kupata maendeleo kwa rahisi zaidi.

Mmoja wa wanufaika wa msaada huo, Schristina Bakari, akiongea kwa niaba ya wenzake alisema jiko hilo linakwenda kumwongezea tija katika upishi wake wa chakula na kuhudumia wateja wake.

"Kwa kutumia jiko hili litanifanya nisinunue kuni kwa ajili ya kupikia ambapo kipindi cha mvua kama hiki kuna wakati tunanunua kuni zikiwa zimenyeshewa wakati wa kusafirishwa na kutusumbua wakati wa kupika, nawashukuru Taifa Gas kwa kututhamini sisi wanawake," alisema.

## Wafanyabiashara watakiwa kusajili biashara zao kisheria

**Na Joseph Mwendapole**

WAFANYABIASHARA mkoani Pwani wametakiwa kusajili bidhaa zao na wenye viwanda wahakikishe wanathibitisha ubora kabla ya kwenda sokoni.

Rai hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Meneja Kanda ya Mashariki Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Noor Meghji, kwenye maonesho ya viwanda na uwekezaji yaliyofanyika mkoani humo.

Aidha, aliwataka wazalishaji wadogo kuthibitisha bidhaa zao, kwa kuwa serikali kupitia TBS inatoa huduma ya bure ya kuthibitisha bidhaa kwa wajasiriamali na kinachotakiwa ni wao kutambuliwa na Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO).

"SIDO ni taasisi mama inayohudumia wazalishaji wadogo, basi itakapokutambulisha kwetu huduma ya uthibitishaji wa bidhaa hiyo unakuwa ni bure, kwa hiyo hakuna sababu yoyote ya kupeleka bidhaa sokoni bila kuwa na nembo ya ubora," alisema Meghji.

Alipongeza jitihada ambazo zimefanywa na Mkuu wa Mkoa wa Pwani kufanikisha maonesho hayo na kwamba TBS imeshiriki ili kuwahimiza washiriki wa maonesho hayo kuzingatia ubora wa bidhaa wanazozalisha.

"Iwapo haujathitibisha ubora wa bidhaa unazozalisha, haujathibitisha ubora wa mifumo, basi biashara na uwekezaji huo hauwezi kuwa endelevu," alisema.

Aliwaeleza washiriki wa maonesho hayo majukumu ya shirika hilo na huduma zinazotolewa na TBS.

Meghji alisema majukumu ya TBS ni kuhamasisha masuala ya viwango, kufanya uthibitishaji wa bidhaa pamoja na mifumo, ukeshaji upimaji wa bidhaa husika, kufanya ukaguzi maeneo mbalimbali yanayohusika na uuzaji na usambazaji wa bidhaa.

Alitaja mengine kuwa ni kusimamia bidhaa zinazoingia nchini kuhakikisha ni zile zenye ubora na salama ndizo zinazoingia nchini kwa kufanya ukaguzi wa bidhaa kabla ya kuingia nchini.

Aidha, Meghji alisema TBS inatoa huduma za kimaabara na lina maabara tisa ambazo zinahusisha upimaji bidhaa mbalimbali.

"Pia tunatoa huduma ya upimaji binafisi kwa wanaohitaji huduma hii, kwa mfano mzalishaji yeyote anayetaka kuuza nje ya nchi kuna huduma TBS tunatoa kuwezesha wazalishaji kusafirisha bidhaa zao kwenda nje," alisema.

"Unaweza kuwa unataka kupeleka bidhaa nje ya nchi ukaambiwa tunataka bidhaa hiyo iwe imetambuliwa na taasisi kutoka nchi yako ambayo inathibitisha ubora na usalama wa bidhaa hiyo, basi TBS tunatoa huduma hiyo," alisema.



# Neema wauzaji mafuta kwenye vidumu

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

WAFANYABIASHARA wadogo wa mafuta kwenye vidumu maeneo ya pembezoni mkoani hapa wanatarajia kupata mkopo kutoka serikalini kwa ajili ya kujenga vituo vya kuuzia nishati hiyo.

Neema hiyo ilitangazwa jana na Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Burian, wakati akizungumza na wakazi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga.

Balozi Batilda, alisema fursa hiyo ni mpango wa serikali wa uwezeshwaji wananchi na kumaliza kilio cha kukosa vituo vya kuuzia mafuta vijijini.

Batilda amedokeza juu ya mkopo huo, ikiwa ni siku chache tangu apokee taarifa ya utekelezaji wa mkakati wa nishati safi ya kupikia iliyozinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan Mei mwaka huu kutoka kwa Wakala wa Umeme Vijijini (REA).

Aliwataka REA kutoa ajira kwa vijana kulingana na teknolojia kwenye utengenezaji wa majiko ya udongo hadi kufikia ya gesi.

"Ajira kwa sasa ni tatizo, tunajua vijana wengi sasa hivi kila mmoja anataka kujiajiri na ni kwa sababu hawezi kupata ajira serikali au taasisi binafsi, hivyo katika kuhakikisha tunawapa ajira, kila teknolojia itakavyobadilika tunaenda nao sambamba" alisema.

Mkurugenzi wa Tekinolojia za Nishati Jadilifu na Mbadala Vijijini, kupitia REA, Advera Mwijage, alisema mradi huo unatekezwa wilaya nane za Mkoa wa Tanga.

Mwijage, alisema katika kuhakikisha wananchi wanaondokana na uharibifu wa mazingira na kulinda afya zao kwa kuepuka uzalishaji wa hewa ya ukaa, serikali kupitia Wizara ya Nishati inasambaza mitungi hiyo kwa wananchi vijijini.

"Kila wilaya itapata mitungi 3,255. Mkoa mzima utapata jumla ya mitungi 26,040 kwa gharama ya shilingi milioni 455.7," alisema.

# Watalii wazidi kumiminika Ngorongoro

**Na Godfrey Mushi,** KARATU

IDADI ya watalii wanaoitembelea Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), imeongezeka hadi kufikia 551,512 katika kipindi cha miezi mitano na kuiingizia serikali mapato ya zaidi ya Sh. bilioni 138.680.

Akizungumza jana wilayani hapa, wakati wa hafla ya kuvishwa cheo na uapisho wa Kamishna mpya wa Uhifadhi wa NCAA, Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, alisema kati ya watalii hao wa nje 350.091 na wa ndani 201.421.

Dk. Chana, alimvisha cheo na kumwapisha Dk. Doriye kwa niaba ya Rais, Samia Suluhu Hassan.

Alisema kwa mwaka huu wa 2024/25, mamlaka hiyo imeonesha kasi nzuri ya ukusanyaji wa mapato na kumuelekeza Kamishna wa Uhifadhi wa NCAA, Dk. Elirehema Doriye kuongeza juhudi katika usimamizi wa fedha hizo za serikali.

Kadhalika alimuelekeza Dk. Doriye, kuimarisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), mahusiano ya kikazi, kusimamia haki za watumishi, mahusiano na wadau na kuongeza hamasa ya utalii wa ndani.

**Akizungumza jana wilayani hapa, wakati wa hafla ya kuvishwa cheo na uapisho wa Kamishna mpya wa Uhifadhi wa NCAA, Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, alisema kati ya watalii hao wa nje 350.091 na wa ndani 201.421.**

Maelekezo hayo yametolewa wakati NCAA imeanza kampeni maalum ya kuchochea ongezeko la watalii wa ndani maarufu kama Merry & Wild, Ngorongoro Awaits.

Kampeni hiyo itawawezesha Watanzania wengi kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo Ngorongoro, urithi wa utamaduni wa Olduvai, Kreta ya Empakai, Olmoti na mlima wa tatu kwa urefu Tanzania wa Loromalasi.

Pia, kuna utalii wa Jiolojia ya Ngorongoro maarufu kama Ngorongoro- Lengai UNESCO Geopark.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurunezi wa NCAA, Jenerali mstaafu, Venance Mabeyo, alimpongeza Dk. Doriye kwa kuteuliwa, kuvishwa cheo, kuapishwa na kumuomba kuendelea kusimamia kikamilifu shughuli za uhifadhi, utalii na maendeleo ya jamii.

Awali, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, , Dk. Hassan Abbasi, alimpongeza Dk. Doriye kwa uteuzi, kuhudhuria mafunzo ya Jeshi la Uhifadhi na kuhitimu.

Dk. Abbasi, aliwataka watumishi wa NCAA kutoa ushirikiano wa kutosha katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi.



Wakazi wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga wakichagua nguo juzi katika gulio la Jumatatu kwa ajili ya sikukuu ya Krismas na Mwaka Mpya. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Waathirika maporomoko Hanang' watoa neno kwa Rais Samia

**Na Allan Isack,** HANANG'

WAKAZI wa Wilaya ya Hanang' mkoani Manyara, wamemshukuru Rais, Samia Suluhu Hassan kwa kuwasaidia baada ya kukumbwa na maafa ya maporomoko ya tope Disemba 3, mwaka jana.

Mbunge wa Hanang', Samwel Hhayuma alitoa shukrani hizo juzi kwa niaba ya wakazi hao, wakati akizungumza kwenye uzinduzi na kukabidhi nyumba 109 za waathirika wa janga hilo katika Kitongoji cha Waret, Kijiji cha Gidagamowd, mbele ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

"Tunamshukuru Rais Samia alikuwa nje ya nchi na kuahirisha ziara yake japokuwa angeweza kutuma mwakilishi ila alifika na kabla aliagiza mawaziri 17 wahamie Hanang' ili kupambana na maafa hayo," alisema Hhayuma.

Alisema ili kuonyesha mapenzi mema waliyonayo wakazi wa Hanang' wametoa zawadi ya ndoo ya lita 20 ya asali kwa Rais Samia na Majaliwa kiasi kama hicho.


Hata hivyo, alisema Hanang' inazidi kupiga hatua ya maendeleo kwenye sekta ya elimu, afya na miundombinu ya barabara.

Mbunge huyo, alitoa ombi mashamba makubwa ambayo hayatumiwi na wawekezaji wapatiwe wakulima kipindi hiki cha kilimo na ugawaji mbegu kwenye ruzuku iwe rahisi kwa kundi hilo ili wanufaike.

Hhayuma, alisema wanahitaji kituo cha kituo cha kupooza nishati ya umeme ili kujenga viwanda vya kusindika chumvi na saruji.

Alisema wakazi hao hawana kitu cha kumlipa Rais Samia za kuahidi kumchagua kutetea kiti hicho katikam Uchaguzi Mkuu mwakani.

Katika makabidhiano hayo ya nyumba hizo na hati za viwanja, wakazi hao pia walipatiwa mitungi ya gesi 109.



# Majambazi wazua taharuki mpakani

**Na Shaban Njia,** NGARA

BAADHI ya wakazi wa Kata ya Mabawe Wilaya ya Ngara mkoani Kagera mpakani mwa Tanzania na Burundi wanadaiwa kukimbia makazi na biashara kuhamishwa kwa kuhofia kuuawa na majambazi.

Hayo yamebaini baada ya Mbunge wa Ngara, Ndaisa Ruhoro kukabidhi mawe kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi cha kata hiyo ili kukabiliana na matukio ya ujambazi ambayo yamekuwa yakitikisa maeneo hayo na kuzua taharuki kwa wakazi hao na wafanyabiashara kwa kuhofia kuuawa, kujeruhiwa na kuporwa mali.

Mmoja wa wakazi hao, Victor Ntamalengero wa Kijiji cha Mlugina Kata ya Mabawe, alisema baadhi ya wafanyabiashara wamelazimika kuhamisha biashara na familia zao kukimbia wahalifu hao.

Ntamalengero, alidai familia zao na wafanyabiashara wamekuwa wakivamiwa, kuporwa mali zao na kuamua kuondoka na kuhamishia biashara zao katika maeneo mengine yakiwamo ya Kata ya Kabanga.

"Mwezi wa tano mwaka huu walivamiwa na majambazi na kuvunja maduka na vioo vya magari na kuiba mali, tulitoa taarifa Jeshi la Polisi na kufika haraka na kufanikiwa kumkamata moja akiwa na silaha. Kujengewa kituo hiki itakuwa ahueni kwetu," alisema.

Jane Mkandala, alidai majambazi walivamia kwenye duka lao na kumjeruhi mwanafunzi kwa kumpiga risasi kwenye paja wakati wakimshurutisha kutoa fedha.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Muruguna kinapojengwa kituo hicho, Erick Mlindwa, alisema wamekuwa wakitoa taarifa kuhusiana na majambazi kuvamia mara kwa mara maeneo yao Kituo cha Polisi Kabanga, lakini wanachelewa kufika na kukuta wamepora mali, kujeruhi na kukimbia.

Diwani wa Kata hiyo, Safari Banigwa alithibitisha baadhi ya wafanyabiashara na wananchi kuhama maeneo yao kwa kuhofia kuendelea kuvamiwa na majambazi, kuuawa na kuporwa mali zao.

Banigwa, alisema wanaendelea kuhamasisha ujenzi wa kituo hicho ili kukabiliana na majambazi kwa kuwa wanatishia kukwama kwa shughuli za kijamii na kiuchumi kwenye eneo lao.

Mbunge Rohoro, alisema serikali iko bega kwa bega na wakazi hao kutatua changamoto zilizopo mbele yao.

Alisisitiza kuwa atahakikisha ujenzi wa kituo hicho unakamilika haraka na kuanza kazi ili kukabiliana na uvamizi unaofanywa na majambazi nyakati za usiku.

Alisema atalishauri jeshi hilo kuruhusu askari wa vituo vyake vilivyopo jirani na kata hiyo kupangiwa kufanya doria mara kwa mara kwenye maeneo hayo hadi ujenzi wa kituo hicho utakapokamilika na kuanza kufanya kazi..

## SHUWASHA kutumia mamilioni mtambo kuchakata tope la kinyesi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA) inatarajia kutumia Sh. milioni 338 kwa ajili ya upanuzi wa mtambo wa kuchakata tope la kinyesi ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira na vyanzo vya maji katika kipindi cha mvua.

Meneja Uendeshaji Miundombinu wa SHUWASA, Mhandisi Wilfred Lameck alitangaza mpango huo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye eneo la upanuzi wa mradi huo lililopo Kata ya Kizumbi Manispaa ya Shinyanga.

Lameck, alisema upanuzi huo unafanyika ili kuongeza kiwango cha uchakataji huo kutoka lita za ujazo 40 hadi kufika lita 100.

Mkurugenzi Mtendaji wa SHUWASA, Yusuph Katopola, alisema mtambo huo ni wa kuchakata tope kinyesi kutoka majumbani na utanufaisha watu 200,000 wa Manispaa hiyo miji jirani.

Katopola, alimwagiza mkandarasi kukamilisha mradi huo kwa wakati kwa kiwango cha ubora kulingana na thamani ya fedha iliyotolewa.

Mkandarasi huyo, Swalehe Maganga wa Kampuni ya Kanuta Engineering Supply, alisema ataukamilisha mradi huo kulingana na mkataba ili kuruhusu wananchi kupata huduma.

**Lameck, alisema upanuzi huo unafanyika ili kuongeza kiwango cha uchakataji huo kutoka lita za ujazo 40 hadi kufika lita 100.**



Mkurugenzi wa kiwanda cha kuchakata samaki cha The Pride of Nile (PVT) kilichopo wilayani Muleba, mkoani Kagera, Manoj Manoharan (kulia), akitoa ufafanuzi kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Dk. Ashatu Kijaji, baada ya kutembelea kiwanda hicho juzi kuangalia shughuli za uzalishaji. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Wasichana Uvinza sasa kupikia majiko ya umeme

**Na Adela Madyane,** KIGOMA

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO) limekabidhi majiko mawili ya umeme yenye thamani ya Sh. milioni 14 katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Uvinza mkoani hapa kwa lengo la kudhibiti matumizi ya nishati chafu ya kuni.

Akikabidhi majiko hayo juzi Mwakilishi wa UNIDO, Doroth Kitutu, alisema wanaunga mkono jitihada za serikali kudhibiti matumizi ya kuni katika taasisi za umma.

Doroth, alisema majiko hayo yametolewa kupitia Mradi wa Pamoja Kigoma (KJP) baada ya kupokea ombi kupitia kikao cha kamati tendaji cha mradi huo.

"Tutaendelea kusaidia kutoa fedha kwenye shule nyingine kadri uwezo utakavyoruhusu," alisema.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Kigoma, Hassan Rugwa, alisema ni wakati wa kushirikiana na wadau kudhibiti uharibifu wa katika mazingira.

Rugwa, alisema lazima tahadhari ichukuliwe kwa kutumia majiko ya nishati safi ya kupikia kwenye taasisi zao ili kuondoa matumizi ya majiko ya kuni ya kupikia.

Alilishukuru shirika hilo kwa msaada huo ambao umelenga kuhifadhi mazingira kwa kudhibiti ukataji miti ovyo kwa ajili ya mkaa na kuni kupikia majumbani .

Ofisa Elimu wa Mkoa huo, Pauline Ndigeze, alisema shule hiyo imeanza kuchukua wanafunzi wa kidato cha tano kuanzia Julai mwaka huu na Januari mwakani itapokea wengine 120 wa kidato cha kwanza.

Ndigeze, alisema kutolewa kwa majiko hayo kunaunga mkono mpango wa serikali wa matumizi ya nishati safi kwenye shule za bweni, kutunza na kuhifadhi mazingira.

Mkurugenzi wa kampuni ya kutengeneza majiko hayo, Atukuzwe Wilson, alisema yanatumia umeme kidogo na kuwataka wananchi wasiogope kununua na kuyatumia ili kunusuru mazingira.

Ukurasa 14



## KWAHERI 2024 ULIITIKISA KARIAKOO UKIKATIZA UHAI WATU 29 NA KUJERUHI

Ukurasa 12



## HERI YA NOELI Sikukuu iwe nguzo ya mahaba, upendo kwa wote

siasa
JUMATANO DESEMBA 25, 2024
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU

### HERI YA KRISMASI: OGOPA

# Desemba isikubadilishe tabia, ukaanza mwaka na kilio

- 'Usharobaro', tambo pesa za mikopo, magari ya kuazima

**Na Mwandishi Wetu**



Furaha ya 'shoping' ya sikukuu , ilingane na mfuko. **PICHA: MTANDAO**

HERI ya sikukuu ya Noeli pamoja ujio wa mwaka mpya. Ni safari za kurudi nyumbani, ukitembelea mitandao ya 'booking' na ukifika vituo vya mabasi unaelezwa kila kitu kimejaa. Watu wanatoka mijini na majiji kwenda vijijini kusherehekea Krismasi, kumaliza mwaka na kuanza mwaka mpya 2025.

Lakini kikubwa ni kutambua kuwa ukitumia pesa nyingi vibaya tena ulizokopa benki, au kwa wakausha damu, ama ndugu au kuweka mali zako rehani kutangaza ufalme vijijini au popote kwa ndugu zako unajidanganya na Krismas na mwaka mpya vitakufundisha adabu au kukutokea puani.

Ni wakati wa kuwa na nidhamu ya fedha na kuacha kununua vitu vingi usivyohitaji na kulewa au kunywa kupindukia, kununua ng'ombe, mbuzi na kuku ukiwafurahisha marafiki kwa lengo la kujitutumua na kutangaza ufalme au usharobaro.

Kuna wengine ili aonekane ni 'kibosile', anaingia kijijini au popote akiendesha magari ya kifahari lakini ya kukodi au kuazima. Ni jambo jema kufanya kile roho inapenda lakini hilo halifai kujifanya mmiliki wa Ford Ranger, Jeep au Hammer ambayo si yako ili marafiki, wanawake na wananchi wakuone uko vizuri kumbe njaa kali.

Kumbukeni kuwa sherehe zinapomalizika unaanza kilio, msongo wa mawazo, maradhi ya afya ya akili baada ya kuwa na wakati mgumu kutokana na kushindwa kulipa madeni makubwa uliyojisababishia kuanzia kukodi magari na mikopo ya fedha za watu uliyochukua.

Utalia zaidi ukishindwa kuwalipia watoto na wategemezi wako ada ya Januari ambayo inaambatana na vifaa vya shule kama sare, magodoro kwa wanaokwenda bweni.

La muhimu sherehe hizi zisiwe za kuendeleza ubadhirifu na matumizi mabaya ya miili yenu kuanzia ngono, ulevi kupindukia, kula mno ambavyo huwaacha watu wengi na uchungu, sonona, shida ya akili baada ya kuchezea fedha kiholela bila sababu na kunufaisha wafanyabiashara mijini na vijijini.

Kuna madai kuwa huu ndio msimu wa ngono. Hilo nalo mabinti na wanafunzi wajiangalie wasijiachie wakawa wameambukizwa maradhi na kupata mimba wakashindwa kusoma Januari 2025.

Baadhi ya wafanyabiashara wa chakula, pombe na nyumba za wageni Manzese jijini Dar es Salaam wanasema msimu wa sherehe hizo ndizo nyakati za kupata fedha kwa sababu ni kama "watu hupata wazimu". Matumizi makubwa ya pombe, chakula na nyumba za kulala wageni yanaongezeka kuliko kawaida.

Wanaiambia Nipashe kuwa wanapata fedha maradufu na mara nyingi malengo ya mauzo wakati huu wa sikukuu ni makubwa na pesa zinapatikana vyakutosha.

Watu wanatumia milioni kadhaa kuanzia mkesha wa Krismasi, hadi mwaka mpya, lakini baada ya hapo wanaanza kuomba mkopo kwa jamaa zao wa vijijini au marafiki hata kuweka mali rehani ili waweze kurudi kazini mijini na kutatua shida zao za kifedha.

Kumbuka ulevi na sherehe husababisha ajali, kuua, kujeruhi na kukamatwa, ukashtakiwa kwa kusababisha yote hayo kisa kuendesha gari kiholela. Kuna uwezekano wa kuishi rumande kwa siku kadhaa maana hakuna anayeweza kukudhamini kwa ujanja na starehe zako.

Usisahau pia kuna uwezekano wa kufukuzwa kwa sababu ya mambo kama hayo ya utovu wa nidhamu. Wakati huna kazi ndio muda wa kampuni za kukodisha magari zitadai fedha zake na wale uliochukua mikopo watakukalia kooni.

Kumbuke ni heri kufunga na kuomba kuliko kujifurahisha kwenye karamu za aina hiyo zinazokuharibia mipango na kuendeleza ulafi. Tena kwenye sherehe hizo ndio wakati wa kusikia taarifa za uharibifu wa mali kuumizana kwenye pombe na kupoteza vitu vya thamani.

Usipoangalia unaweza kuuza mali kama nyumba na mashamba kufidia mali za watu hasa fedha na magari ulizokopa au kuharibu.

Aidha, Desemba ndio ambao kukopesha pesa kunanoga, wazee wa kausha damu wanakuwa kazini kwao ni mwezi wa 'kumeki' na kupata faida, anadokeza mjasiriamali anayetoa mikopo eneo la Mwenge Dar es Salaam.

"Wanaofanya biashara hii ya kukopesha fedha hawana tatizo na wazee wa matumizi wanachotafuta kwako ni fedha zako tu. Lazima uweke dhamana nono wewe mteja wetu na kupewa riba kubwa ili usipotimiza ahadi wajue namna ya kukukamua au kukukausha damu." Anasema jina lake na kampuni tunalitunza kuheshimu wateja wake.

Anaongeza "Hawaangalii wanaacha laptop, simu za thamani, vito hasa dhahabu na tanzanite, nguo za bei ghali na wengine samani. Sisi hatuna shida..." anasema.

Kumbukeni ukosefu wa nidhamu ya pesa ndicho chanzo cha mambo hayo ambayo wengi hayawasaidii.

**TAHADHARI MVUA**

Kuna taarifa za mvua kubwa wilayani Same mkoani Kilimanjaro na pia mikoa ya Rukwa na Katavi, hivyo watu wanaposherehekea siku kuu wasisahau taarifa za Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA).

Ni vyema kuchukua tahadhari ya mvua wakati wa sikukuu katika maeneo mbalimbali usijisahau mafuriko na vimbunga havijua Krismas tena havina mwaka mpya.

Mvua kubwa zinaambatana na ngurumo na radi, hivyo wakazi katika maeneo yenye mvua za vuli wawe macho kwa kuwa ajali zinaweza kutokea na kuwa misiba badala ya sherehe.



Upendo kwa watoto wanaoishi nje ya familia na mazingira hatarishi ni jambo linalosisitizwa wakati wa sikukuu ya Noeli na Mwaka Mpya. **PICHA: MTANDAO**

WANAWAKE WASEMA

# Sikukuu iwe nguzo ya mahaba, upendo kwa wote

**NA MWANDISHI WETU**

LEO ni Krismas, Jarida la Siasa linawatakia wasomaji wetu, siku kuu njema zenye furaha na amani. Tukitakiana heri hizi kunaambatana na kukumbushana kuwa sherehe hizi zilizoanza usiku wa kuamkia leo hadi tarehe 31, kisha Januari mosi 2025 zisiwe mwanzo wa kufanya maovu.

Baba na mama lakini pia wachumba acheni kuchepuka au kukosa uaminifu. Anza Krismasi, maliza mwaka huu na anza mwaka mpya mkiwa mnathaminiana kila mara.

Mama kubali kuwa maandalizi aliyoyafanya mume wako kwa sikukuu ndio uwezo wake, tumieni mlicho nacho kwa furaha. Kama ni mama watoto au mchumba pia mkubali hali zenu. Kinachotakiwa ni kudumisha mapenzi na kujali.

Jihadharini msiingie kusaka wapenzi wengine kipindi hiki cha sikukuu kisa kutafuta pesa zaidi.

Wanawake na wanaume wafahamu kuwa nyama ya ulimi ni muhimu wakati wote hata kama mume hana kitu ni muhimu kuongeza upendo na kutiana moyo.

Kwa upande wa wanaume hata kama unaona kuna kasoro kwa mkeo ni muhimu kumpenda. Mpigie simu baba au mama watoto wako au mwenza wako na hata mchumba wakati wote uonyeshe kuwa unajali kwa kujuliana hali iwe mchana asubuhi na hata jioni kabla hajarejea nyumbani.

Katika msimu huu wa sikukuu, maisha ya watu hayawezi kubadilika kwa muda mfupi, hivyo kama hujajaliwa kupata pesa za maandalizi upendo unaweza kuwa silaha ya kuziba udhaifu wenu.

Jitahidini kuvumiliana na kukubali kuwa maisha si pesa pekee, mapenzi kwa wanandoa, wachumba pamoja na upendo kwa familia na ndugu bila kusahau amani ya roho na akili timamu vikiongozwa na hofu ya Mungu vinashinda yote.

Wanandoa kama mmekuwa mkikwaruzana kila wakati, kipindi hiki mnatakiwa kuondoa uhasama kwa kuwa huu ndio wakati mzuri wa kunyoosha mapito na kuwa mwanzo wa kuombana msamaha na kuona raha ya ndoa.

Kumuomba mpenzi wako msamaha sio ishara ya udhaifu, bali kiungo muhimu cha kukoleza penzi lenu kwa baba na mama pamoja na familia yenu.

Kama mhimili wa familia, baba chukua nafasi yako kwa kununua vyakula hata kama ni kabichi ili familia ipate faraja. Ukitaka kupalilia vyema penzi, wanaume ni vizuri mkawasindikiza wake zenu sokoni kununua vitu iwe kuku, kabichi, vitunguu na mchele kutegemea ukwasi wenu.

Haitakua jambo baya kwa wanaume mkiwasindikiza wenza wenu saluni ili wajirembe kwa kusuka nywele kwa ajili ya sikukuu. Kadhalika baba awahudumie watoto wako wanunulie nguo mpya watoto kama pesa zipo.

Zawadi nzuri hupewa mkeo au mwenza wako, lakini hilo halitakulazimisha kama hauna uwezo.

> "Familia ziandae chakula siyo kuwaachia watoto wazurure majumbani na kula kwa watu wengine. Waache kusema atakula kwa majirani si kulinda watoto kwanini uwaache kwa majirani?" Anahoji.

Baba na mama kumbuka mambo madogo ambayo watu hupuuza ndio hukoleza raha na mapenzi katika msimu huu wa sherehe za sikukuu za Noeli, kumaliza na kuanza mwaka mpya.

Askofu Waliam Mwamalanga, wa Kanisa la Kipentekoste Tanzania , anakumbusha kuwa maana ya Siku ya Noeli ni upendo wa Mungu kwa mwanadamu na kwamba ni muhimu mwanadamu anayependwa na Muumba atende upendo huo kwa vitendo.

Katika salamu zake za Krismas, Askofu Mwamalanga, anasema kila mtu amwendee mwenzake hasa wale wanaokaa na chuki na kinyongo kwa muda mrefu asalimiane naye kumaliza chuki iwe ni mke au mume, jirani, watoto na wazazi au walezi.

Anashauri wawapelekee chochote cha thamani na kuwapa hasimu wao ikiwa ni pamoja na kununua kitu kizuri na kuwapatia wale ambao hawawapendi na kufungua ukurasa mpya wa upendo na amani.

Askofu Mwamalanga anakumbusha kuwa kwa wakati huu ambao hali imekuwa ngumu, vilio vya maisha magumu na watu wamefariki kwenye ajali, kila mmoja awe mlinzi wa mwenzake na kutiama moyo. "Tujali watoto hata kama hatujawazaa na tuhudumie wale ambao hatuwajui." Anasisitiza.

Kuhusu kujiburudisha anashauri watu wanywe vinywaji laini kama soda, juisi, pia wale matunda na vyakula vyenye lishe kwa sababu pombe kali wamezitumia mwaka mzima. Wawe makini walinde familia zao.

"Familia ziandae chakula siyo kuwaachia watoto wazurure majumbani na kula kwa watu wengine. Waache kusema atakula kwa majirani si kulinda watoto kwanini uwaache kwa majirani?" Anahoji.

Anashauri sherehe za Noeli na mwaka mpya ziwe za mabadiliko kwa watoto zianze kwa walezi na wazazi kuwavisha mavazi yenye heshima.

"Wajihisi wafalme wajione wana walezi na wazazi. La muhimu tuwahudumie watoto wasio na msaada mitaani. Na sisi twende kuwatembelea wanaoishi kwenye mazingira magumu na familia maskini popote walipo. Tupeleke upendo." Anashauri Askofu Mwamalanga.

MPENDE 'HAUSI GELI'

Ofisa Miradi wa Asasi ya Initiative for Domestic Workers inayotetea watumishi wa nyumbani wilayani Bagamoyo mkoa wa Pwani, Farida Daniel, anakumbusha kuwa kipindi hiki mabosi wawaonyeshe kuwajali wafanyakazi wa ndani na si kuwabagua.

Anawashauri waajiri kuwapa muda wa kupumzika na kufurahia sikukuu za Noeli na mwaka mpya, akiwakumbusha kuwa wapende watoke na watoto wao kufurahia.

"Kuna wengine wanawatumikisha kuanzia saa 11 alfajiri hadi saa 4:00 usiku ni kazi pekee. Ahudumie wageni, aandae vyakula na mwisho hafurahii Noeli wala mwaka mpya." Anashauri Farida.

Anawashauri watumishi hao kutimiza wajibu kwa kufanyakazi kwa wakati, kupanga ratiba zao na kufuata maelekezo na si kusikiliza wale wanaowapotosha.

NA DK. FELICIAN KILAHAMA

### DIWANI KULISHWA MATOPE

# Viongozi wajihoji iwapo wao ndio tatizo au shida ni fedha

## •Kama ni pesa na mipango zipo zilizorudishwa Hazina

WIKI iliyopita Desemba 18, zinasikika taarifa kuwa wananchi wamemburuza diwani wao kwenye matope na sababu ya kufanya hivyo zikatajwa kuwa ni kutoridhishwa na utendaji wake, hali mbaya ya barabara katika eneo lao na kwa kifupi kutokuwajibika.

Ukweli ni kwamba hata sehemu wanazoishi watu wengine wengi hali za barabara hasa nyakati za mvua ni 'kichefuchefu' pamoja na kero nyingi mitaani. Kuna wanaotupa taka bila kujali usafi wa mazingira na kutiririsha majitaka ovyo nyakati za mvua ikiwamo kufungua makaro ya taka za vyooni.

Kadhalika, akasikika 'kiongozi kigogo' akitoa pongezi tena, akisifia kitendo kilichofanywa na wananchi wa eneo hilo kwa diwani wao nikabaki nimeduwaa kidogo nikijiuliza kufanya hivyo ni sahihi?

Hata hivyo, kiongozi huyo shupavu akaongeza kusema 'viongozi wengi hawawajibiki ipasavyo' nami nakubaliana na hoja hiyo.

Hali ya viongozi kutowajibika kikamilifu, inapelekea wananchi kushikwa na hasira na kufanya maamuzi magumu kama hilo la kuburuzana kwenye mapote. Kadhalika, akaongeza kuwa mwaka wa fedha 2023/2024 kiasi cha shillingi bilioni 20 zilirudishwa hazina, kisa hazikutumika wakati zilitakiwa zitumiwe kuwaletea maendeleo au kuimarisha huduma za kijamii katika halmashauri husika.

Baada ya tafakuri fupi ndipo nikawaza je, tatizo au changamoto Tanzania ni upatikanaji wa fedha au ni ukosefu wa uongozi imara? Kufikiri ni kitu kimoja na matokeo yake ni kitu kingine. Hata hivyo, sikuwa na jibu kamili.

Kwanza, utwala, uongozi wa nchi umejengeka kwenye misingi ya sheria na katiba ya Tanzania ikiwa ndiyo sheria kuu ikifuatiwa na sheria, kanuni na taratibu za kisekta, kisiasa na kitaaluma. Vilevile, kuna viongozi wa kisiasa na wa kiutendaji lakini pia wapo wataalamu kutokana na taaluma mbalimbali zikiwamo za kijamii, kisiasa, kisayansi, kisaikolojia, kidini na mifumo ya kijadi pia.

Taifa hili ni tajiri na siyo maskini hivyo fedha na rasilimali nyingine kuanzia watu, ardhi na mazao vyote ni fedha toshelezi, changamoto zilizopo zinatokana na binadamu wenyewe. Mathalani, kama halmashauri ikipokea fedha ilizoomba kuwaletea maendeleo na kuimarisha huduma za kijamii katika eneo lake kulingana na mipango iliyopeleka serikali kutoa hizo fedha; halafu zisitumike hadi kurudishwa, ni jambo la kutatanisha.

Je, kulikuwa na makosa katika kupanga maana ni pamoja na kuchagua nini cha kufanya, nini kisifanyike, iweje zisitumike ilivyotarajiwa? Wananchi wanaposikia fedha nyingi kiasi hicho hazikutumika wakati uhalisia wa mambo katika maeneo mbalimbali kwenye sehemu zao ni 'kero' tupu zisizopata ufumbuzi wa haraka, inasababisha 'sintofahamu' hadi kufanya maamuzi yasiyofaa ambayo pia ni kinyume na utawala wa kisheria.

Viongozi wa sekta na wizara mbalimbali, mashirika, mikoa na halmashauri Tanzania Bara, nimekuwa nikiwasikia wakisema "... namshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, Mama yetu mpendwa amekuwa akitoa fedha nyingi kuwaletea maendeleo Watanzania..."

Hili kisiasa ni sawa, lakini kiutendaji pamoja kwamba Rais ni Mtendaji (Executive President) lakini mifumo ya kiutawala na kiutendaji ipo hivyo, inatakiwa ifanye kazi ipasavyo. Mathalani, bunge la bajeti likipitisha makadirio na matumizi ya fedha kwa mwaka husika hutayarishwa muswada wa fedha ambao ukiridhiwa na wabunge na hatimaye kuwekwa saini na Rais, inakuwa ndiyo sheria ya fedha kuhalalisha matumizi ya kiasi kilichopitishwa na bunge kwa mwaka huo.

Baada ya hapo, wizara, mashirika, mikoa, halmashauri pamoja na bunge na mahakama huanza kutekeleza shughuli zilizoanishwa kwa kutumia fedha zilizoidhinishwa. Kupitia Sheria ya Fedha kwa kupindi husika.

Hata hivyo, katika kuwahangaikia wananchi wa maeneo tofauti Rais, anaweza akapata fedha au misaada kutoka nchi marafiki au hapa nyumbani ambazo ni nje ya bajeti na kwa matashi yake akazitoa zitumike kwa faida ya wananchi wa eneo fulani.

Ikitokea ikawa hivyo, hata mimi nisingesita kumshukuru kwa jitihada kama hizo zenye dhamira njema kwa Watanzania.

Viongozi wa kisiasa kama madiwani na wabunge kupitia maeneo yao wanawajibika kukusanya kero na kuzifanyia kazi na kukazana fedha zitapatikane kupitia bajeti za serikali, ili kuondoa kero za wananchi kwa kutumia fedha zilizoidhinishwa rasmi au zilizopatikana kihalali kupitia mifumo tofauti.

Iwapo hatua hazichukuliwi haraka na kero kukithiri sehemu kadhaa nchini motokeo ni mfano wa barabara mbovu kupelekea wananchi kumwadhibu diwani kinyume na sheria na taratibu. Kimsingi, wanaorudisha fedha bila kuzitumia ilivyotarajiwa siyo wanasiasa bali viongozi watendaji iwe wizarani au kwenye halamashauri husika.

Ukifuatilia jambo lilo utagundua ni watumishi na watendaji wa umma wenye mizozo binafsi itokanayo na migongano ya kimaslahi kiasi cha kuwaadhibu wananchi kwa kutotumia fedha zilizoidhinishwa zitumike kuwaondolea kero sehemu husika.

Miaka ya karibuni 'pepo' la ubinafsi na kutowajibika ipasavyo kwa baadhi ya viongozi wa umma limekuwa changamoto kubwa kwenye usimamizi wa rasilimali fedha katika sekta ya umma. Fedha zikitolewa na hazina au kama inavyosemwa na Rais, zitumike kulingana na kusudio lenyewe mfano, kujenga au kuimarisha miundombinu ya barabara, kilimo, umwagiliaji, kusambaza maji au umeme, afya na elimu kwa jamii mijini na vijijini.

Kusiwepo na 'roho' kwa baadhi ya viongozi kutaka kujinufaisha wanapohoji nafsini mwa fedha zikitumika binafsi nitapata nini na au nitafaidika vipi? Hizo ni 'roho' zilizojaa 'uovu' zinazofurahia au kushabikia 'kero na mateso' kwa wananchi wakati wenyewe watendaji na watumishi wanatakiwa kuwajibika kuwatumikia wananchi ipasavyo.

Nionavyo mimi suala la kurejesha bakaa ya fedha kila mwisho wa mwaka wa fedha wa serikali ni la kiutendaji si la kisiasa. Lakini inapotokea fedha zikarejeshwa kuwepo sababu za msingi zisizoepukika kiutendaji au kiutawala.

Inapotokea kushindwa kutumia fedha zilizoidhinishwa na bunge zisitumike kwa sababu baadhi ya viongozi na watendaji wanakwamisha na kupelekea suala hilo kutokea kinyume na matarajio ya wananchi kwa kujali maslahi binafsi kuliko ya umma na taifa kwa ujumla, huo ni 'ufisadi' mkubwa hatua kali zichukuliwe.


Kadhalika, vyombo vya habari na mitandao ya kijamii vinasema mgonjwa analetwa kwenye zahanati, kituo cha afya au hospitali akiwa mahututi, lakini wataalam husika wanakataa kumtibu wakidai malipo kwanza na kusababisha kifo. Watanzania utu na kuthaminiana pia kuhurumiana na kupendana kama binadamu vimepotelea wapi au ndiyo matokeo hasi ya utandawazi, kupenda fedha sana kuliko ubinadamu?

Kimsingi viongozi, watumishi wanaoteuliwa kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma kwenye wizara, mashirika, mikoa, wilaya na halmashauri wawe watumishi wenye mioyo iliyobeba maslahi ya umma na taifa kuliko maslahi binafsi.

Kiongozi wa aina hiyo hatafurahia kurudisha fedha hazina wakati eneo analolisimamia limesheheni kero lukuki hivyo atafanya kila linalowezekana fedha zitumike kihalali na kwa faida ya wengi.

Viongozi 'kutunishiana misuli' haina tija kwa jamii pia wananchi na viongozi kuburuzana kwenye matope au kukejeliana siyo jambo jema. Isipokuwa wote kwa pamoja tunatakiwa tushirikiane na kufanya kila linalowezekana kuhakikisha kila Mtanzania anaishi kwa amani na kupata mahitaji ya msingi mfano, chakula, mavazi, mahali pa kuishi, afya njema, kufanyakazi kwa bidii.

Watoto wakipata elimu stahiki na miundombinu kujengwa ipasavyo kote nchini. Fedha ziwe na matokeo chanya ya jasho letu na kila mtu akijivunia kipato halali pamoja na kuwa na hofu ya Mungu.



Ni msoto kwa wakazi wa Msumi na Madale Dar es Salaam, kusafiri kutokana na kukosa daraja kwa mwaka sasa. **PICHA: MTANDAO**

KWAHERI 2024

# Uliitikisa Kariakoo ukikatiza uhai watu 29 na kujeruhi

## •Kuteka na kuua, buriani mwana CHADEMA Ali Kibao




Maafa ya Kariakoo yaliyoua watu 29. : **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**NA MWANDISHI WETU**

SAFARI ndefu ya siku 365 1/4 ya mwaka 2024 iliyojaa milima na mabonde inaelekea ukingoni ili kuukaribisha mwaka mwingine wa 2025 ambao unatarajiwa kuanza Jumatano ya wiki ijayo.

Mwaka 2024 ulikuwa na matukio mengi makubwa yaliyoibua mijadala na hisia mchanganyiko miongoni mwa Watanzania, kuanzia katika siasa na hata vifo vya baadhi ya watu wenye majina makubwa ndani na nje ya nchi.

Baadhi ya matukio katika siasa, yanaanza na Dk. Emmanuel Nchimbi kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa CCM kuchukua nafasi iliyoachwa wazi na Daniel Chongolo aliyejiuzulu mwishoni mwa mwaka 2023. Kwa sasa Chongolo ni mkuu wa mkoa wa Songwe.

Ilikuwa ni Januari 15, 2024 Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM inapokea na kuidhinisha pendekezo la Kamati Kuu ya chama hicho la kumteua Balozi Nchimbi kuwa Katibu Mkuu wa CCM.

Uamuzi huo ulifikiwa katika kikao maalum kilichoketi Zanzibar kikiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Taifa Rais Samia Suluhu Hassan.

Juni 30, mwenyekiti wa zamani wa Kanda ya Nyasa wa CHADEMA ambaye pia ni mbunge wa zamani wa Iringa Mjini, Peter Msigwa anatangazwa rasmi kuhamia CCM kwenye kikao cha Halmashauri



Jenerali David Musuguri

Kuu ya CCM Taifa jijini Dar es Salaam.

Viongozi kujiuzulu na safari hii Julai 29, Makamu Mwenyekiti wa CCM Abdulrahman Kinana, anajiuzulu nafasi hiyo Julai 29,2024. Ombi lake linaridhiwa na Mwenyekiti wa Taifa, Rais Samia.

Agosti mosi mwaka unashuhudia wakili Boniface Mwabukusi akichaguliwa kuwa Rais wa Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS), baada ya kupitia misukosuko mingi ikiwamo ya kuenguliwa katika kinyang'anyiro na kukimbilia mahakamani.

Panga pangua ya baraza la mawaziri ilisikika kila wakati. Agosti 14, aliyekuwa Waziri wa Afya Ummy Mwalimu anatumbuliwa, huku nafasi yake ikichukuliwa na Jenista Mhagama ambaye awali alikuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu).

Novemba 27, uchaguzi wa serikali za mitaa unarindima na CCM inashinda viti vingi, lakini ushindi huo unalalamikiwa kila kona na wadau mbalimbali wa siasa na demokrasia, wakiwamo wanaharakati na viongozi wa dini.

Habari za wasiojulikana kuteka zinazidi kuzagaa, ni Desemba mosi Mwenyekiti wa Ngome ya Vijana ya ACT Wazalendo, Abdul Nondo anadai kukamatwa na kuchukuliwa kwa nguvu na watu sita.

Ni tukio la dakika chache baada ya kuwasili katika stendi kuu ya mabasi ya Magufuli Mbezi Dar es Salaam akitokea Kigoma alipokuwepo kikazi.

Desemba 2, Jeshi la Polisi linathibitisha kuwa Nondo amepatikana baada ya kutelekezwa eneo la fukwe za Coco Dar es Salaam akiachwa na watu asiojulikana.

Taarifa hiyo inaeleza kuwa Nondo alisimsimamisha bodaboda na kumuelekeza amfikishe katika ofisi za chama chake Magomeni na kufika saa 5:00 usiku na kuonana na viongozi



Abdul Nondo, Mwenyekiti wa Ngome ya Vijana **ACT –Wazalendo**

wake kabla ya kupelekwa hospitali kwa ajili ya uchunguzi wa afya..

Desemba 17, Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Tundu Lissu anachukua fomu kugombea nafasi ya mwenyekiti wa chama hicho taifa huku akiwajibu watu wanaokosoa uamuzi wake kuwa jambo hilo si la ajabu na kuwahoji walitaka achukue nani.

Ilipotimia Desemba 21, Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, anachukua fomu ili kutetea nafasi yake hiyo inayoishikilia kwa miaka mingi, kitendo ambacho kinaonyesha kutakuwa na ushindani mkali kati ya viongozi hao wawili wenye ushawishi mkubwa ndani na nje ya chama hicho.

Kitendo cha wababe hao kuchukua fomu ili kuwania nafasi moja, kimeibua makundi mawili ya wanachama na wafuasi wa chama hicho ambao sasa wamegawanyika pande mbili kitendo kinachoashiria kuwa uchaguzi wa mwenyekiti wa CHADEMA taifa utakuwa na ushindani mkali.

**MATUKIO YA VIFO**

Mwaka umewaachia majonzi wengi, na kubwa ni Novemba 16, Dar es Salaam na taifa vinazizima kwa msiba, kufuatia kuporomoka kwa ghorofa Kariakoo na kusababisha vifo vya watu 29 waliokuwa wakifanya shughuli mbalimbali za kibiashara.

Usiku wa kuamkia Novemba 27, ulijaa simanzi baada ya Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Dunia (WHO) Kanda ya Afrika na mbunge wa Kigamboni Dk. Faustine Ndugulile, kufariki dunia ghafla kabla hajaanza kutumikia nafasi mpya ya kimataifa.

Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali David Musuguri (104) , anaaga dunia mwaka huu Oktoba 29, akipatiwa matibabu katika hospitali jijini Mwanza.

Septemba 6, mjumbe wa Sekretarieti ya CHADEMA Taifa, Ally Mohamed Kibao, anafariki dunia akidaiwa kutekwa na watu wasiojulikana waliomshusha katika basi la Tashriff akiwa Tegeta Dar es Salaam, safarini kwenda Tanga, kitendo ambacho kilizua sintofahamu kwa Watanzania, wadau wa siasa na hata leo hakuna aliyekamatwa.

Oktoba 12, Brigedia Meja Jenerali mstaafu Charles Mbuge, aliyewahi kuwa Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na pia mkuu wa mkoa wa Kagera, anafariki dunia, akiwa kwenye matibabu nchini India.

Novemba 9, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, Lawrence Mafuru, anaaga dunia wakati akiendelea kupatiwa matibabu nchini India.

Ajali nazo hazikuicha Tanzania salama, Desemba 22, watu 11 waliokuwa wakisafiri kwa basi wilayani Biharamulo mkoani Kagera walifariki.

*Heri ya Noeli na pole kwa walioumia moyo mwaka 2024.*





## "Tukemee ukatili wa kijinsia makanisani, misikitini"

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

VIONGOZI wa dini wametakiwa kukemea vitendo vya ukatili wa kijinsia miongoni mwa waumini wao kwenye nyumba za ibada badala ya kuiachia serikali ili vitokomezwe katika jamii.

Wito huo ulitolewa juzi na Kasisi wa Kanisa la Aglikana Tanzania Parishi ya Kikuyu jijini hapa, Gershon Maloda, wakati akizungumza na waumini wa kanisa hilo ikiwa ni sehemu ya kampeni maalum ya kuelimisha jamii athari za vitendo hivyo.

Maloda, alisema kuwa suala hilo ni mtambuka, hivyo viongozi hao wanapaswa kukemea kwa waumini wao ambao ni miongoni mwa jamii, ambako vitendo hivyo vinaendelea kukithiri kila kukicha ili iendee kuishi katika hali ya amani, utulivu na upendo.

"Suala la ukatili wa kijinsia ni mtambua, kila mtu anao wajibu wa kukemea kwani hawa wanaofanya vitendo hivi ni waumini wetu tuponao ndani ya nyumba zetu za ibada, hatuna budi kukemea tabia hii ili ikome," alisema.

Akizungumizia vitendo hivyo, alisema katika makanisa wamekuwa wakipokea malalamiko mengi kutoka kwa wanandoa ya vipigo.

"Hivi sasa kanisa tunapokea malalamiko sana kutoka kwa wanafamilia hasa vipigo kwa wanandoa, wenza kunyimana unyumba, kundi jingine ni wadada wa kazi na watoto ndani ya familia.

"Kutokana na hali hiyo tumekuwa tukifundisha waumini wetu kuzingatia maandiko matakatifu kumaliza vitendo hivi, lakini kwa wasichana wa kazi tunazungumza na waumini wetu kuwachukulia kama binadamu wenzao na siyo kuwanyanyasa kwa vipigo ama kuwatesa kwa namna yoyote," alisema na kuongeza kuwa:

" Pia watoto wetu ndani ya familia zetu hawapaswi kulala chumba kimoja na ndugu yoyote yule."

Katibu na Mratibu wa Maendeleo ya Umoja wa Kinamama wa Kanisa la Aglikana Tanzania (UMAKI), Magreth Ndonde, alisema lengo la kampeni hiyo ni kuunga mkono juhudi za serikali kukabiliana na ukatili wa kijinsia nchini.

"Sisi kama kanisa tumekuwa tukiungana na wadau wengine kila mwaka kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia, mwaka huu tumeamua kutoa elimu kwa waumini wetu ndani ya nyumba za ibada kupata uelewa wa athari za ukatili wa kijinsia," alisema.

Alisema kampeni hiyo itakuwa endelevu ili kuwafikia waumini wengi na kukomesha vitendo vya ukatili wa kijinsia nchini.

# Prof. Makubi: BMH kuwa hospitali ya taifa 2025

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKURUGENZI Mtendaji wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Benjamin Mkapa (BMH), Profesa Abel Makubi, ametaja vipaumbele vikuu vitatu vya utekelezaji wa hospitali hiyo kwa mwaka 2025, ikiwamo kuipandisha hadhi kutoka kanda na kuwa ya taifa ili kuboresha huduma zaidi kwa wananchi.

Profesa Makubi alisema hayo jijini hapa katika mkutano na watumishi wa hospitali hiyo wa kufanya tathmini ya utendaji kazi, utoaji huduma, usimamizi na uendeshaji kwa kipindi cha miezi sita kuanzia Julai hadi Desemba mwaka huu.

Alisema watumishi wote wa hospitali hiyo wanapaswa kujipanga na kujiandaa kwa utekelezaji wa vipaumbele hivyo katika kipindi cha mwaka huo mpya unaotarajiwa kuanza siku chache zijazo.

"Waziri wa Afya na Katibu Mkuu wote walifika BMH na kuonyesha umuhimu mkubwa kuwa Hospitali ya Taifa, hivyo ni jukumu letu uongozi na watumishi wote kuboresha zaidi utendaji wetu ili kukamilisha azma hiyo," alisema Profesa Makubi na kuongeza kuwa:

"Tumeweka mikakati mwakani kuanzia Januari kuhakikisha vipaumbele vyote vilivyotajwa vinatekelezwa ipasavyo ili kuhakikisha tunafanikisha malengo tuliojiwekea."

Alitaja vipaumbele vingine kuwa ni kuendelea kuboresha maslahi ya watumishi, kupandisha madaraja, kuwawezesha kujiendeleza kielimu, kuwapa mafunzo ya kuwajengea uwezo na motisha wanapofanya vizuri.

Vilevilile, alisema kipaumbele kingine ni kuendelea kusimamia, kukamilisha miradi ya maendeleo inayotekelezwa na BMH ili kuongeza na kuboresha huduma zinazotolewa kwa jamii kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Profesa Makubi, alisema katika kuongeza na kuboresha zaidi mazingira ya utoaji huduma, wanatakiwa kujipanga ili kuhakikisha wanakamilisha miradi ya huduma ya maji, ujenzi wa kituo kikubwa cha tiba ya saratani kwa awamu mbili.

Aliwataka wajumbe wa menejimenti na watumishi wa BMH kusimamia vizuri majukumu ya uendeshaji, usimamizi na utoaji huduma ili kufikia malengo yao.

Katika hatua nyingine; Profesa Makubi amewapongeza watumishi hao kwa utendaji kazi na kuwahimiza kuongeza bidii zaidi ili kufikia malengo.



Ikeam Mnyani mkazi wa Kipunguni jijini Dar es Salaam akiuliza swali katika mafunzo ya kujua sheria mbalimbali yaliyofanyika kwenye viwanja vya Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni yakitolewa na watumishi wa Dawati la Msaada wa Kisheria Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wafanyakazi wapewa motisha

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

OFISI ya Mkuu wa Mkoa wa Singida imetoa zawadi kwa watumishi wake ili kuonesha upendo, kuwajali na kuwapa motisha katika utendaji wao kuelekea Sikukuu ya Krismasi, leo na mwaka mpya 2025.

Watumishi hao walikabidhiwa sukari, mafuta ya kula, mchele, vitenge na fedha taslimu juzi na Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa huo, Stanslaus Choaji.

Akizungumza baada ya kukabidhi zawadi hizo, Choaji, alisema tukio hilo limefanyika kwa lengo la kuthamini mchango watumishi kwa ushirikiano walioonesha kuwatumikia wananchi katika kipindi cha mwaka huu na kufikia malengo.

"Zawadi hizi ni sehemu ndogo ya kuthamini uwepo wa watumishi wote kwa kuonyesha ushirikiano ambao umezaa matunda ya mafanikio kuhakikisha Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida inafanya kazi kwa weledi kuwahudumia na kuwafikia wananchi wake kwa wakati," alisema.

Choaji, alisema motisha kwa watumishi hautafikia tamati badala yake utaendelea kutolewa kila mwaka na kuboreshwa zaidi ili waendelea kuwa na morali.

Ofisa Utumishi Ofisi ya Mkuu wa Mkoa huo, Josephine Mbozu, akizungumza kwa niaba ya watumishi hao, aliushukuru uongozi wa Sekretarieti chini ya Mkuu wao, Halima Dendego na Katibu Tawala, Dk. Fatuma Mganga kwa kuwajali na kuutambua mchango wao katika utendaji kazi.

"Tunashukuru kwa zawadi ya Krismasi, zimetufaa na familia zetu, tunasema asante kwa upendo wenu, Mwenyezi Mungu awabariki sana kwa kutujali," alisema.

Katibu wa Madereva ofisi ya Mkuu wa Mkoa huo, Ismail Shamakala, alisema ni faraja kwa viongozi kuwathamini watumishi kwa kuwapa motisha.

Shamakala, alisema zawadi hizo zimewapa chachu kuzidi kuipenda kazi yao kwani mahusiano kati yao na viongozi ni mazuri na mazingira ya kazi ni ya furaha na amani.



# TAZARA yapewa somo mishahara wafanyakazi

**Na Nebart Msokwa,**
TUNDUMA

NAIBU Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile, ameuagiza uongozi wa Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) kuandaa mpango ili kuweza kulipa mishahara wafanyakazi wake kwa kusafirisha shehena ya mizigo kati ya nchi hizo na za Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC).

Kihenzile alitoa agizo hilo alipotembelea kituo cha reli hiyo kilichopo mjini hapa Mkoa wa Songwe kwa lengo la kukagua uendeshaji wa reli hiyo kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Zambia.

Aliwataka viongozi kuwa wabunifu wakati serikali inaendelea kutatua matatizo yanayoikabili mamlaka hiyo ya uchakavu wa baadhi ya miundombinu, kushindwa kulipa mishahara na kukosa shehena ya mizigo ya kusafirisha na kulazimika kutumia barabara.

Alisema kitendo cha reli hiyo kufanya vibaya kinasababisha matatizo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukwama shehena kubwa za mizigo kusafirishwa na wafanyakazi kukosa mishahara kwa sababu ya kushindwa kujiendesha.

Alisema ili kukabiliana na tatizo hilo, viongozi hao wanatakiwa kubuni njia za kisasa za kuendesha mamlaka hiyo ili iwe na uwezo wa kujiendesha kwa faida na kuchangia kwenye pato la taifa kwa kutoa gawio.

"Kitendo cha shirika (mamlaka) kuto 'operate' (kutofanya kazi), kinasababisha serikali kukosa fedha ambazo zinatokana na usafirishaji wa mizigo, nawaombeni sana muwe wabunifu, leteni mpango kazi wa uendeshaji wa reli hii kisasa," alisema Kihenzile.

Vilevile alisema kitendo cha reli hiyo kutofanya kazi ipasavyo kinasababisha barabara kuharibika kwa kusafirisha mizigo ambayo ilitakiwa isafirishwe kwa treni.

Hata hivyo, alisema mataifa jirani hasa yaliyoko ukanda wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ambayo hayana bandari, yanashindwa kusafirisha mizigo yao kutoka katika Bandari ya Dar es Salaam kwenda kwao na mataifa mengine.

Meneja wa TAZARA Tanzania, Fuad Abdallah, alisema serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 2.5 kwa ajili ya kujenga njia mbili za reli katika kituo hicho cha Tunduma na kununua vifaa vya kisasa vya kukagua mizigo.

Alisema wamenunua vifaa vya kisasa kwa ajili ya kukagua abiria na mizigo na kuzuia kutumika kusafirisha vitu visivyostahili kwenda mataifa jirani.

Alisema vifaa hivyo vimenunuliwa kwa kituo hicho kwa sababu kipo mpakani mwa nchi hizo kufanya ukaguzi kama kwenye viwanja vya ndege na bandarini.

Aliwaomba wadau wa usafirishaji wa mizigo kuendelea kuiamini mamlaka hiyo kwa kusafirisha mizigo yao kwa kuwa usalama umeimarishwa.



Baadhi ya wanachama wa vikundi vya wanawake na vijana Kata ya Msoko, wilayani Rungwe mkoani Mbeya, wakiwa wamejitwisha mizinga ya nyuki jana baada ya kukabidhiwa na halmashauri kwa ajili ya kuiweka kwenye misitu na vyanzo vya maji ili kulinda mazingira. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wagawiwa mizinga kufugia nyuki

**Na Nebart Msokwa,**
RUNGWE

HALMASHAURI ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya imeanza kugawa mizinga ya nyuki kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili kuwakwamua kiuchumi na kuondokana na umaskini kupitia mazao ya nyuki na utunzaji wa mazingira.

Vikundi hivyo vinavyopatiwa mizinga hiyo vinatakiwa kuiweka kwenye misitu iliyohifadhiwa na vyanzo vya maji ili kuhakikisha maeneo hayo yanaendelea kuwa salama.

Kaimu Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya hiyo, Numwagile Bughali, alisema mizinga hiyo ni sehemu ya asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri hiyo ambayo kwa mujibu wa sheria inatakiwa kutolewa kwa makundi hayo maalumu.

Bughali, aisema lengo la halmashauri hiyo ni kugawa mizinga zaidi ya 200 kwenye kata zote na kwa kuanzia 50 imetolewa kwa vijiji vya Syasya na Igembe vilivyopo Kata ya Masoko.

Alisema baada ya kukamilisha kwenye kata hiyo, wanakusudia kuendelea kugawa kwenye kata nyingine hasa zile ambazo zina misitu iliyohifadhiwa na serikali.

"Mizinga hii ni sehemu ya utekelezaji wa sheria, tunaamini itakuwa ni chanzo cha uhakika cha mapato yenu maana mtakuwa mnavuna asali na mazao mengine ya nyuki na kuuza," alisema Numwagile.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Mpokigwa Mwankuga, alivitaka vikundi vilivyopatiwa mizinga hiyo kuzingatia maelekezo ya wataalamu ili vifanye vizuri kwenye utekelezaji wa miradi yao.

Mwankunga, alisema vikundi walivyoanza kuvipatia ni vile vya mfano na kwamba wataendelea kuvifuatilia ili vikifanya vizuri viongezewe mizinga mingine.

Alisema lengo la serikali kutenga asilimia 10 ya mapato kwa ajili ya vikundi hivyo ni kuhakikisha inawainua wananchi hasa walio kwenye makundi maalumu kiuchumi wasiendelee kuwa tegemezi kwa jamii inayowazunguka.

Wakizungumza baada ya kukabidhiwa mizinga hiyo, baadhi ya wanufaika hao, waliishukuru serikali na kuahidi kuitunza ili izalishe na kutimiza lengo la kuwainua kiuchumi na kutunza mazingira.

Mmoja wa wanufaika hao, James Mwakangale, alisema kabla ya kupewa mizinga hiyo, walikuwa wanaendelea na ufugaji wa nyuki kwa kutumia mizinga michache na kuishukuru serikali kwa kuwaongezea mtaji.

Mwakangale, alisema tangu walianze kufuga nyuki, wameanza kuona matunda na ni sababu ya kuomba mingine kwenye halmashauri baada ya serikali kurejesha mikopo ya asilimia 10.

Tedy Mwakisopo, mfugaji wa nyuki katika Kijiji cha Syasya, alisema wakati wanaanza mradi huo wananchi walikuwa hawaamini kwamba wangefanikiwa kutokana na imani shughuli hiyo ni ya wanaume.

# Kituo cha afya sasa chajengewa barabara

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

WAKALA wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) wilayani hapa Mkoa wa Njombe, umeanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kwenda Kituo cha Afya Mtwango kwa gharama ya shilingi bilioni moja.

Hayo yalisemwa juzi na Mbunge wa Lupembe, Edwin Swalle baada ya kufanya ziara ya kukagua ujenzi wa barabara hiyo yenye urefu wa kilomita moja akiwa ameambana na viongozi wa Chama Cha Mapunduzi (CCM) na serikali.

Swalle, aliwataka wananchi kuwa wavumilivu wakati mradi huo unaendelea kutekelezwa katika eneo hilo.

Alisema kukamilika kwa mradi huo kutarahisisha usafiri kwa wagonjwa kwenda kituoni hapo na kuokoa maisha yao baada ya kufika kwa wakati kupata huduma.

"Barabara hii ni muhimu kwa sababu itawasaidia wagonjwa, wajawazito na watoto ambao walikuwa wakiathirika pindi wanapofuata huduma hasa msimu wa mvua za masika," alisema Swalle.

Alitoa rai kwa mkandarasi kukamilisha mradi huo kwa miezi sita kulingana na mkataba ili wananchi waanze kuitumia.

Kwa upande wake mkandarasi huyo wa kampuni HKS Laboratory Civil and Building Contractors Ltd, Hassan Nyoni alimwakikishia mbunge huyo atafanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa mujibu wa mkataba.



## Spika aimwagia sifa sekta ya utalii Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SPIKA wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Ali Maulid, ameisifu sekta ya utalii kwa kuendelea kupokea wageni wengi kutembelea vivutio vilivyoko visiwani hapa na kuiongezea serikali mapato.

Spika Maulid alitoa kauli hiyo wakati wa uzinduzi wa mradi wa Hoteli ya Mzuri Villa Sort iliyopo Fukuchani Mkoa wa Kaskazini Unguja, ikiwa ni shamrashamra za Maadhimisho ya Miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar .

Alisema mradi huo una lengo la kuhakikisha watalii wanaofika Zanzibar wanapata hifadhi za malazi zenye mandhari nzuri wanapokuwa mapumzikoni.

Maulid, alisema serikali imewawekea mazingira mazuri wawekezaji wakubwa katika sekta ya hoteli ili kuinua sekta hiyo.

"Kwa kweli Serikali ya Zanzibar inafanya kila jitihada kuwawekea mazingira mazuri wawekezaji wake na hii ni faraja kwa wao, " alisema .

Alisema takwimu zinaonesha kuwa idadi ya watalii wanaoingia visiwani hapa inazidi kuongezeka mwaka hadi mwaka kutoka na sekta hiyo kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo maeneo mbalimbali.

Maulid, alisema takwimu hizo zinaonesha kuwa mwaka jana, Zanzibar ilipokea watalii 640,000 na kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii.

Alisema idadi hiyo inaweza kuongezeka na kufikia lengo la sekta hiyo kupokea watalii milioni moja.

Spika huyo, alisema serikali imeendelea kuweka mazingira mazuri ya kisera na kisheri kuongeza wigo wa sekta ya malazi kwa kuibua miradi mingi ya ujenzi wa nyumba za biashara kwa wageni.

"Kuibuka kwa miradi mingi kumechangiwa kwa kiasi kikubwa na shauku kubwa ya wageni kupendelea kuishi kwa muda mrefu katika mandhari mazuri ya visiwa vyetu," alisema.

Alisema kuwa uwekezaji wa sekta ya ujenzi wa nyumba za biashara kwa wageni nchini ndio uwekezaji wa pili unaongoza kwa kuleta mitaji mikubwa nchini ikifuatiwa na uwekezaji wa sekta ya mahoteli.

Alisema takwimu zinaonesha kuwa asilimia 37 ya miradi yote ya uwekezaji iliyosajiliwa na Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa serikali ya awamu ya nane ni ya hoteli ikifuatiwa na asilimia 22 ya nyumba za biashara.

Mkurugenzi Mkuu Mtendaji wa ZIPA, Salehe Saad Muhamed, alisema kwa kipindi cha miaka minne mamlaka hiyo imesaini miradi 424 Zanzibar yenye thamani ya dola bilioni 5 .9.

Muhamed, alisema kwa Kaskazini Unguja miradi 99 imetoa ajira 22,000.

Mwekezaji wa mradi huo, John Godson Mabwambo, alisema hadi kufikia sasa mradi huo una vyumba vya biashara 22 na wafanyakazi 17 .

# Serikali ya Zanzibar kuboresha miundombinu ya mahakama

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imesisitiza kuwa itaendelea kuboresha miundombinu ya majengo ya Mahakama na utendaji kazi wake ili kuharakisha usikilizaji kesi na kuondoa manung'uniko kwa wananchi.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyasema hayo wakati akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa jengo la Mahakama ya Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja katika eneo la Mazizini visiwani hapa.

Dk. Mwinyi, alisema SMZ imefanikiwa kuleta mageuzi kwenye majengo ya mahakama visiwani hapa kwa kutoa fedha za ndani kwa asilimia100.

Alisema mageuzi hayo yana lengo la kutoa huduma bora kwa wananchi katika mazingira ya kuridhisha na kuujengea heshima muhimili huo.

"Tumetumia fedha zetu wenyewe kwa sababu tungesubiri za wafadhili tungechelewa kufikia mafanikio haya," alisema Dk. Mwinyi.

Akizungumzia jengo la zamani la Mahakama ya Vuga, alisema litaendelea kuwa la Mahakama na kuridhia azma ya kulifanya kuwa Makumbusho ya Mahakama.

Alisema kwa miaka mingi muhimili huo umekuwa ukitekeleza majukumu yake kwenye majengo chakavu.

"Palipo na majengo mazuri, lazima huduma bora zipatikane. Nimeridhishwa na mabadiliko makubwa ya utendaji wa Mahakama visiwani hapa kwa sasa," alisema.

ilevile, Dk. Mwinyi, alisema SMZ inatarajia kujenga jengo jingine kubwa litakalokuwa na Mahakama ya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi.

Aliyataja majengo mengine yatakayojengwa kwa nguvu ya serikali kuwa ni pamoja na Mahakama ya Wilaya Makunduchi, Mahakama ya Wilaya ya Magharibi A Kijichi, Mahakama ya Watoto Mahonda na Mahakama ya Wilaya ya Wete, Pemba.

Alisema majengo hayo mapya yatakuwa na huduma za teknolojia ya kisasa.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Jaji Mkuu wa Zanzibar, Khamis Ramadhan Shaaban, aliipongeza serikali kwa kufanikisha ujenzi wa jengo hilo kwa muda mfupi.

Mtendaji Mkuu wa Mahakama visiwani hapa, Kai Bashir Mbarouk, alisema ujenzi huo una lengo la kuboresha upatikanaji haki kwa wakati na kuondoa malalamiko ya wananchi wanaofika mahakamani hapo kusikiliza kesi zao.

Mbarouk, alisema ujenzi wa jengo hilo umefikia asilimia 85 na litakuwa na huduma zote za mahakama.



Vijana wakibeba mizigo ya wateja kuwapelekea nje kutokana na magari ya kushusha bidhaa kuongezeka kuelekea sikukuu ya Krismasi katika soko la Mabibo, Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# SUZA yatakiwa kuongeza juhudi kwenye utafiti

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande, amekitaka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kuongeza juhudi kufanya utafiti kwa manufaa ya wananchi.

Chande alitoa rai hiyo katika mkutano wa pili wa mkusanyiko wa kitaaluma uliofanyika Chuo cha Utalii Maruhubi visiwani hapa.

Alisema kuwa utafiti wa kina unaofanywa na taasisi za elimu ya juu kama SUZA ni muhimu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi kukuza maendeleo nchini.

Alisema kuwa imezoeleka kuwa tafiti zinafanywa kwa kutumia fedha nyingi na muda, lakini zinaishia katika makabati ya ofisini.

Chande, alisema ni wajibu tafiti hizo kufanyiwa kazi kama ilivyo kusudiwa kwa manufaa ya taifa na wananchi.

Alisema chuo hicho kipo mstari wa mbele kutoa vijana wengi na kuwa wataalamu wa fani.

"Wakati umefika sasa kwa wataalamu kufanya kazi kwa maslahi ya taifa na kuondoa ubinafsi," alisema Naibu Waziri huyo.

Aliwataka wahitimu wa chuo hicho kuchangamkia fursa za ajira ili kuendelea kuijenga Zanzibar katika nyanja zote.

"Wataalamu wanaomaliza katika chuo hiki wanatakiwa kuwa wakakamavu na kuchangamkia fursa ili kuendelea kuvipatia maendeleo Visiwa vya Zanzibar," alisema.

Mwenyekiti wa Mkusanyiko wa Kitaaluma ambaye ni Waziri wa Maendeleo, Jinsia, Wazee, Wanawake na Watoto, Riziki Pembe Juma, alisema mkusanyiko huo wa wanataaluma unamanufaa makubwa kwa vijana wanosoma katika chuo hicho ili kuwa viongozi wazuri kwa baadaye.

Makamu Mkuu wa SUZA, Profesa Makame Haji, alisema tangu kuanzishwa kwa chuo hicho maendeleo makubwa yamepatikana, ikiwepo kutoa wataalamu wazuri katika fani mbalimbali ili kuwa viongozo bora wa baadaye.

# Rais aunda Tume kutathmini mgogoro wa ardhi Ngorongoro

**Na Christina Mwakangale**

TUME ya Rais ya Kutathmini kuhusu Mgogoro wa Ardhi katika Hifadhi ya Ngorongoro, iliyoundwa na Rais Samia Suluhu Hassan, imeundwa na wajumbe 10, huku ikiongozwa na Jaji wa Mahakama ya Rufani, Dk. Gerald Ndika.

Taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Dk. Moses Kusiluka, ilisema kwamba, Rais Samia baada ya kuunda Tume hiyo, amemteua Jaji Ndaki kuwa Mwenyekiti pamoja na wajumbe 10.

"Desemba Mosi, 2024 Rais Samia Suluhu Hassan alipokutana na viongozi wa kimila wa jamii ya kimasai wanaoishi eneo la Hifadhi la Ngorongoro alitangaza uamuzi wa serikali kuunda Tume mbili.

"Tume ya kwanza itafanya tathmini kuhusu masuala ya ardhi yanayolalamikiwa na wakazi wa Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na Tume ya pili itaangalia utekelezaji wa uhamaji wa hiari kutoka eneo la hifadhi hiyo," alisema Kusiluka. Wajumbe walioteuliwa ni pamoja na Philemon Luhanjo; Zakia Hamdani Meghji; Jaji George Masaju ambaye ni Jaji wa Mahakama Kuu na Mshauri wa Rais, Sheria; Dk. Richard Muyungi, Mshauri wa Rais, Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi; Balozi Salome Sijaona; Prof. Wilbard Kombe wa Chuo Kikuu Ardhi.

Wengine ni Prof. Emmanuel Luoga wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA); Mollel James Moringe, ambaye ni Diwani na Katibu wa Baraza la Wafugaji Ngorongoro; Moi Aprakwa Sikorei, Diwani na mkazi wa Ngorongoro.

Kadhalika kwenye Tume ya Kutathmini Zoezi la Uhamaji wa Hiari wa Wakazi wa Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Rais Samia, amemteua Mhandisi Musa Iyombe, Katibu Mkuu mstaafu kuwa Mwenyekiti wa Tume hiyo, ikiwa na wajumbe wanane.

Wajumbe hao ni Sihaba Nkinga; Alphayo Kidata, Mshauri wa Rais, Uwezeshaji Biashara na Masuala ya Kodi; Balozi Valentino Mlowola; Balozi Mohamed Mtonga; Balozi George Madafa; Haruna Masebu; Edward Maura Nduleti, Diwani na Mwenyekiti wa Baraza la Wafugaji Ngorongoro na Rehema Moisare, Mwalimu na mkazi wa Ngorongoro.



Mkurugenzi wa Utawala na Raslimaliwatu wa Hospitali ya Benjamini Mkapa, Prisca Lwangli (kulia), akikabidhi tuzo ya mshindi wa kwanza ya usimamizi bora wa raslimaliwatu kwa Mkurugezi Mkuu wa hospitali hiyo, Profesa Abel Makubi, wakati wa mkutano mkuu wa wafanyakazi wa hospitali hiyo uliofanyika mjini Dodoma jana. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

## DC apongeza kamati ya lishe kuleta matokeo chanya

**Na Benny Kingson, TABORA**

MKUU wa Wilaya ya Igunga mkoani Tabora, Sauda Mtondoo, amewapongeza wajumbe wa kamati ya lishe wilaya kwa kuja na bajeti ambayo italeta matokeo chanya kwenye afya za wananchi.

Sauda alitoa pongezi hizo wakati wa kikao cha mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya Kamati hiyo kwa mwaka wa fedha 2025 hadi 2026.

Alisisitiza kuwa bajeti waliopanga ikatoe matokeo chanya kwa jamii kwa lengo la kupunguza utapiamlo, magonjwa yanayotokana na ukosefu wa lishe.

"Fedha hii iliyotengwa ni nyingi, hivyo hatuwezi kuzungumzia uchumi au maendeleeo kama afya zetu haziko vizuri, afya inaanzia kwenye lishe," alisema.

Alisema mtu akiwa na lishe bora hata magonjwa ya ovyo yanamwepuka, anatamani iwe jamii yenye lishe bora kwa lengo la kuhakikisha inaepukana na magonjwa na kujikita katika shughuli mbalimbali za uzalishaji mali.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuboresha uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla, na kwamba wataalamu wawe na ubunifu utakaoleta matokeo chanya.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Joseph Mafuru, aliwashauri Wakuu wa Idara za Elimu kuyatumia maeneo ambayo yapo karibu na shule yalimwe kuhakikisha chakula kinapatikana na wanafunzi wanakula na kunywa uji wawapo shuleni.

Mkuu wa Idara ya Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe, Lucia Kafumu, aliwashauri Maofisa Lishe kuwa na ubunifu wa kuanzisha bustani ya lishe, kuuza maziwa na kufuga kuku.

Kafumu aliwahimiza kuendelea kuboresha mpango wao kuhakikisha unajibu changamoto kwenye mambo ya lishe na kuleta tija na mafanikio.

# Mvua yakata mawasiliano kata tano saa 72

**Na Mary Mosha, SAME**

MVUA inayoendelea kunyesha wilayani Same, mkoani Kilimanjaro imesababisha kukatika kwa daraja ya Kizangaze na kukata mawasiliano kati ya kata ya Maore, Ndungu, Kihurio, Bendera na kata ya Miamba kwa saa 72.

Pia imesababisha vifo vya watu sita wakiwamo wawili wa familia moja huku baadhi ya wananchi wakiachwa bila makazi baada ya nyumba zao kuangukiwa na ngema.

Wakizungumza jana na Nipashe baadhi ya wananchi walisema mvua hiyo imechangia kupotea kwa ndugu zao pamoja kusombwa kwa mazao shambani.

"Hatuna mawasiliano toka juzi, wasafiri wameshindwa kusafiri, maiti zinavushwa kwenye maji kwa shida, hakika ni adha kubwa, hasa msimu wa mvua," alisema Ally Yusufu.

Naye Diwani Kata ya Maore, Rashid Juma, alisema kukatika kwa daraja hilo kumesababisha wananchi kutembea zaidi ya kilomita 60 kufuata huduma za afya katika Hospitali ya Wilaya ya Same badala ya kilomita tatu kutoka Kituo cha afya cha Ndungu.

"Kwa sasa watu tunakabiliwa na matatizo mengi, ya kukosa usafiri kwenda kituo cha afya, kupeleka mazao sokoni huko ndiko iliko sheli (kituo cha mafuta) kikubwa ambacho tunakitegemea," alisema.

Baadhi ya abiria waliokwama ni wa kwenda Dar es Salaam, Tanga na Morogoro, lakini kwa sasa ili uende huko ni lazima urudi Same ndipo uanze safari na nauli zimepanda hasa kipindi cha mwisho wa mwaka," alisema Juma.

Alisema kukatika kwa daraja hilo sio mara ya kwanza kukatika na kuiomba serikali kuangalia suluhisho la kudumu.

Akitoa jitihada za kazi wanazofanya, Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Mkoa Kilimanjaro, Mhandisi Benitho Mdzovela, alisema katika jitihada za awali kurudisha mawasiliano, wameweka bomba, kalavati za plastiki tatu kila moja lina kipenyo cha mita moja na nusu.

Alisema zitasaidia kupitisha maji kwa dharura na baadaye wanatarajia kujenga daraja la kudumu.

"Mvua imesababisha kukatika kwa mawasaliano kwa kuvunja kuta ngumu za daraja, kwa sasa tunategemea kutumia milioni zaidi 30 na mawasiliano yatarejea baada ya siku mbili.

Alipotembelea daraja hilo na kujionea hali halisi ya uharibifu, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alitoa mkono wa pole wa Shilingi milioni tatu na kuwataka wananchi kuondoka maeneo hatarishi.

"Nawaagiza viongozi wetu kuanzia ngazi ya kijiji hadi wilaya kushuighulikia maeneo hatarishi na kuwashawishi wananchi kuondoka maeneo hayo ili kuepuka madhara yanayoweza kutokea hasa ya vifo na uharibifu wa mali," alisema Babu.

HABARIKIMATAIFA

# Chapo mshindi urais Msumbiji

**MAPUTO, Msumbiji**

BARAZA la Katiba nchini Msumbiji limeidhinisha matokeo ya uchaguzi wa rais yaliyompa ushindi mgombea wa chama tawala cha Frelimo, Daniel Chapo, huku wasiwasi ukiendelea kutanda katika miji mikubwa ya taifa hilo, baada ya kiongozi wa upinzani Venancio Mondlane kuapa kuanzisha vuguvugu la maandamano.

Ilielezwa kuwa hatua hiyo inauweka umma wa Msumbiji katika hali ya wasiwasi, kutokana na upinzani kuonyesha dhamira ya kuanzisha vurugu kupinga uamuzi huo wa baraza la katiba kumwidhinisha Chapo kama mshindi wa uchaguzi wa urais.

Ilielezwa kuwa katika jitihada za kuimarisha usalama mjini Maputo vifaa vya kivita vimewekwa tayari na hakuna mtu anayeweza kuingia au kutoka mjini humo.

Pia ilielezwa kuwa kiongozi wa upinzani Mondlane ameshawaambia wafuasi wake wajiandae kufanya maandamano makubwa yatakayolemaza shughuli zote nchini humo kufuatia uamuzi huo wa baraza la katiba.

Mchambuzi wa masuala ya kisiasa na kiusalama Johann Smith, kabla ya kutangazwa uamuzi wa baraza la katiba alisema kwamba miji mikubwa ikiwamo mji mkuu Maputo huenda ikawa chini ya waandamanaji.

Awali mchambuzi huyo alisema anaamini kwa asilimia 100 kwamba baraza la katiba, litayaunga mkono matokeo yaliyompa ushindi Daniel Chapo wa chama tawala cha Frelimo na kwamba damu lazima itamwagika nchini humo.

Matokeo ya awali yaliyotangazwa na tume yalimpa ushindi Chapo kwa asilimia 71 huku Mondlane akipewa nafasi ya pili akitajwa kupata asilimia 20 ya kura.

Hata hivyo, mgombea huyo wa upinzani anadai yeye ndiye mshindi kwa mujibu wa zoezi jingine lililofanywa pembeni la kuhesabu kura linaonesha alipata asilimia 53 ya kura na Chapo alinyakuwa asilimia 36.

Mondlane amedai matokeo yalichakachuliwa kumpendelea mgombea wa chama tawala cha Frelimo.

Ripoti zinasema kwamba maduka na maeneo ya biashara yamefunga milango yao na mitaa ya mji mkuu Maputo imebaki mitupu licha ya kwamba ni kilele cha kuingia kwenye msimu wa sikukuu ya Krismasi.

Vilevile, ilielezwa kuwa barabara kuu za kuelekea katikati ya mji huo zimefungwa kwa vizuizi vya polisi huku zile za kuelekea ikulu na maeneo ya ofisi za baraza la katiba nazo zikiwa pia zimefungwa.

Nchi hiyo ya Kusini mwa Afrika iko kwenye hali ngumu ya machafuko ya kisiasa tangu tume ilipotangaza matokeo ya uchaguzi uliofanyika Oktoba 9, mwaka huu yaliyompa ushindi mgombea wa chama cha Frelimo ambacho kiko madarakani tangu mwaka 1975 nchi hiyo ilipopata uhuru wake kutoka kwa Wareno.

Polisi wamekuwa wakituhumiwa kutumia risasi za moto dhidi ya waandamanaji na kwamba takribani watu 130 waliaminika kuuawa kwa mujibu wa shirika la kiraia la Plataforma Decide ambalo takwimu zake ndizo zinazotumiwa na shirika la kutetea haki za binadamu la kimataifa la Amnesty International.

***DW***



Rais mteule wa Msumbiji, Daniel Chapo kutoka chama tawala cha Frelimo aliyetangazwa na Baraza la Katiba kushinda uchaguzi wa urais wa Oktoba 9, mwaka huu akiwa na mkewe Gueta Chapo. **PICHA: MTANDAO**

# Israel yathibitisha kumuua kiongozi wa Hamas

**JERUSALEM, Israel**

WAZIRI wa Ulinzi wa Israel, Yoav Galant kwa mara ya kwanza amekiri kuwa Israel ilimuua kiongozi wa kisiasa wa Kundi la Hamas Ismail Haniyeh mjini Tehran mwezi Julai, mwaka huu.

Kiongozi huyo alitoa maoni hayo jana katika hotuba yake akiahidi kuwalenga wakuu wa vuguvugu la Houthi linaloungwa mkono na Iran nchini Yemen, ambalo limekuwa likirusha makombora na ndege zisizo na rubani dhidi ya Israel.

Ilielezwa kuwa Haniyeh aliuawa katika jengo alimokuwa akiishi katika mji mkuu wa Iran katika shambulizi linalohusishwa na Israel. Wakati huo huo, Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu alisema baadhi ya hatua zimechukuliwa katika kukubaliana kusitisha mapigano huko Gaza na Hamas, lakini hakuweza kutoa ratiba ya lini makubaliano yataafikiwa.

Hayo yanajiri baada ya ofisa mkuu wa Palestina kuiambia BBC kwamba mazungumzo kati ya Hamas na Israel yamekamilika kwa asilimia 90, lakini masuala muhimu yalisalia.

Katika hotuba ya waziri huyo alisema Israel itatekeleza mashambulizi makali dhidi ya Houthis na kukata kichwa uongozi wake.

"Kama tulivyofanya kwa Haniyeh, Yahya Sinwar na Hassan Nasrallah huko Tehran, Gaza, na Lebanon, tutafanya hivyo huko Hodeida na Sanaa," alisema, akimaanisha viongozi wa Hezbollah na Hamas ambao wote wameuawa mwaka huu.

Haniyeh (62), alizingatiwa pakubwa kuwa kiongozi wa jumla wa Hamas na alichukua jukumu muhimu katika mazungumzo yenye lengo la kufikia usitishaji vita katika Ukanda wa Gaza.

Baada ya mauaji yake, Hamas ilimtaja Yahya Sinwar, kiongozi wake huko Gaza na mmoja wa wasanifu wakuu wa mashambulizi ya Oktoba 7, kuwa kiongozi mkuu wa kundi hilo.

Sinwar aliuawa na jeshi la Israel katika pambano la kubahatisha huko Gaza mwezi Oktoba na kundi hilo bado liko katika harakati za kumchagua kiongozi mpya.

Hassan Nasrallah wakati huo huo aliyekuwa kiongozi wa kundi la Lebanon linaloungwa mkono na Iran la Hezbollah, aliuawa mjini Beirut mwezi Septemba wakati Israel ikizidisha kampeni yake ya kijeshi dhidi ya Hezbollah, ambayo ilikuwa ikiishambulia kila siku kwa kuvuka mpaka siku moja baada ya shambulio la tarehe 7 Oktoba.

Waasi wa Houthi, ambao wanadhibiti kaskazini magharibi mwa Yemen, walianza kushambulia meli za Israel na kimataifa katika Bahari Nyekundu muda mfupi baada ya Israel kuanza kulenga Hamas huko Gaza Oktoba iliyopita, huku wakiapa kuendelea hadi vita huko Gaza viishe.

***BBC***

# Afrika Kusini yazuia malori kuingia Msumbiji

**CAPE TOWN, Afrika Kusini**

UONGOZI wa Afrika Kusini umepiga marufuku na kusitisha kuingia kwa malori katika kivuko cha mpaka cha Lebombo na Msumbiji kuanzia jana kutokana na wasiwasi wa kiusalama.

Hatua hiyo imejiri baada ya Msumbiji kukabiliwa na machafuko ya maandamano makubwa tangu mwishoni mwa mwezi Oktoba mwaka huu wakati mamlaka ya uchaguzi ilipomtangaza Daniel Chapo, mgombea urais wa chama tawala, mshindi katika uchaguzi wa urais, baada ya madai ya wizi wa kura.

Baraza la Katiba, mahakama ya juu zaidi nchini humo, ilithibitisha jana matokeo ya uchaguzi ambayo yaliongeza utawala wa chama cha Frelimo madarakani kwa nusu karne.

Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Mipaka ya Afrika Kusini (BMA), Mike Masiapato, ilisema "kusimamishwa kwa trafiki ya malori kutaendelea hadi tutakapopewa hakikisho kwamba ukanda huo unalindwa na wanajeshi pamoja na polisi wa upande wa Msumbiji".

Pia kamishna huyo alisema ni magari madogo tu na watu wataruhusiwa kuvuka mpaka na kuingia Msumbiji.

Aidha, alieleza kuwa uamuzi huo ulifanywa kabla ya tamko la Baraza la Katiba la Msumbiji, huku ikielezwa kuwa Lebombo ndio kivuko kikuu cha mpaka cha usafirishaji wa bidhaa na mizigo kati ya nchi hizo mbili.

Ilielezwa kuwa mwezi uliopita Afrika Kusini ilitangaza kufungwa kwa muda kwa kivuko cha mpaka chenye shughuli nyingi kutokana na ghasia zinazoendelea baada ya uchaguzi nchini Msumbiji.

***TRT***

**Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Mipaka ya Afrika Kusini (BMA), Mike Masiapato, ilisema "kusimamishwa kwa trafiki ya malori kutaendelea hadi tutakapopewa hakikisho kwamba ukanda huo unalindwa na wanajeshi pamoja na polisi wa upande wa Msumbiji".**

# AZAM FC 'YAMFUNGA' MASUDI MPAKA 2027

**Na Faustine Feliciane**

UONGOZI wa klabu ya Azam FC umetangaza kumwongezea mkataba golikipa wake namba mbili Zuberi Masudi utakaomweka klabuni hapo mpaka 2027.

Golikipa huyo mkataba wake ulikuwa unamalizika Januari, 2025 na sasa ataendelea kuitumikia timu hiyo mpaka mwaka 2027.

„Golikipa wetu Zuberi Masudi ataendelea kusalia kwenye klabu yetu mpaka mwaka 2027 baada ya kumwongezea mkataba mpya wa miaka miwili, tunamtakia kila la heri kwenye majukumu yake," ilisema taarifa ya klabu hiyo.

Azam imeendelea kuwaongezea mkataba wachezaji wake muhimu kwa ajili ya kuendelea kuitumikia timu hiyo.

Msimu huu Zuberi ametumika kwenye michezo mitano ambapo hajaruhusu bao lolote katika michezo hiyo.

Azam FC kwa sasa inashika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi baada ya kucheza michezo 15 na kufikisha pointi 33 wakilingana na Yanga wanaoshika nafasi ya pili nyuma ya vinara Simba wenye pointi 34 (kabla ya mchezo wao wa jana dhidi ya JKT Tanzania).




Meneja wa RTA Group, Kigambo Abdalah (kulia), akikabidhi sehemu ya msaada kwa mlezi wa kituo cha watoto wenye uhitaji cha Msongola, Christina Haule kwa ajili ya sikukuu za mwisho wa mwaka jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# KenGold kuongeza wachezaji 10

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya KenGold imesema itaongeza zaidi ya wachezaji 10 kwenye kikosi chao katika dirisha dogo la usajili linaloendelea ili kukifanya kuwa imara zaidi kuelekeza mzunguko wa pili wa Ligi Kuu.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Jose Mkoko, amesema usajili huo utafanyika baada ya Kocha Mkuu, Omari Kapilima kukifanyia tathmini kikosi hicho na kuwaambia mabosi wake kuwa anahitaji wachezaji ili kukiboresha baada ya kushika nafasi ya mwisho kwenye msimamo wa ligi baada ya kumalizika kwa mzunguko wa kwanza.

"Tutasajili wachezaji kadhaa, nadhani 10 hivi au zaidi kutokana na mapendekezo ya kocha, kikubwa wachezaji watakaosajiliwa ni wale wenye viwango vya hali ya juu na wazoefu kwenye ligi, ili kukabiliana na ushindani mkubwa iliopo hivi sasa," alisema Mkoko.

Kocha aliyeipandisha daraja timu hiyo na kuanza kucheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza msimu huu, Jumanne Chale, amesema sababu kubwa ya KenGold kutofanya vyema ni aina ya wachezaji wengi iliyonao na inatakiwa kusajili baadhi ya wachezaji watakaokuja kuiinua toka hapo ilipo na kuibakisha kwenye ligi msimu huu.

Alisema kumekuwa na ushindani mkubwa wa ligi msimu huu huku timu nyingi zikiwa zimewekeza pesa nyingi kwenye usajili kwa kuleta wachezaji bora kutoka nje ya nchi.

"Ligi yetu nayo imekuwa ngumu sana, timu zimewekeza kwa kusajili wachezaji bora na wengi kutoka Afrika Magharibi, hii imefanya timu zingine kuwa kwenye wakati mgumu," alisema kocha huyo za zamani wa timu hiyo.

Mara baada ya kumaliza mzunguko wa kwanza, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Kapilima amesema safu yake ya ulinzi iliwaangusha hivyo lazima waongeze nguvu.

"Tumemaliza mzunguko wa kwanza kwa kucheza mechi 15, bado michezo mingine 15, hivyo nafasi ya kubaki Ligi Kuu ipo kama tunafanya marekebisho kwenye safu yetu ya ulinzi kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili," alisema.

Tayari klabu hiyo, imewaacha wachezaji watano ambao ni Steven Mganga, Amir Njeru, Castor Posta, Adam Uledi na Salum Idrissa.

## Wachezaji Mashujaa wakiri ugumu wa ligi msimu huu

**Na Mwandishi Wetu**

WACHEZAJI wa Mashujaa FC, wamekiri kuwa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu imekuwa ngumu na bora zaidi, huku wakijipongeza kwa kukusanya pointi nyingi zaidi tofauti na zile walizopata msimu uliopita walipomaliza mzunguko wa kwanza.

Wakitoa tathmini ya timu yao ya ligi kwa ujumla baada ya kumaliza mechi za mzunguko wa kwanza, baadhi ya wachezaji hao, Crispin Ngushi, Balama Mapinduzi na Erick Johora ambao wote wamewai kuichezea Yanga kwa misimu tofauti, wamesema wanatarajia ugumu zaidi mzunguko wa pili, hivyo kwa sasa wapo kwenye mazoezi makali kujiandaa na mechi zinazofuata.

"Tumekusanya pointi zetu za mazunguko wa kwanza tunashukuru Mungu, si haba, nguvu zetu sasa tunazieleza mzunguko wa pili kwa sababu ndipo inapochanganya na inakuwa ngumu, hata timu ambazo zilionekana dhaifu zinakaza kwa sababu zinahitaji pointi ili kujiweka vizuri kwenye malengo yao, lakini pia zinakuwa zimeshafanya usajili wa dirisha dogo, tumejiandaa vizuri kupata pointi nyumbani na ugenini," alisema Ngushi ambaye anacheza nafasi ya ushambuliaji.

Kiungo mshambuliaji wa timu hiyo, Balama Mapinduzi, amesema msimu huu wamefanya vyema zaidi kuliko msimu uliopita kwani walikuwa wamekusanya pointi tisa tu hadi ulipomalizika mzunguko wa kwanza, lakini msimu huu wamemaliza wakiwa na pointi 19.

"Msimu huu ligi imekuwa na ushindani mkubwa, timu nyingi zipo vizuri na zinatamani kila mchezo ipate matokeo ya ushindi.

Msimu huu tumejipanga vizuri tofauti na msimu uliopita ambapo kipindi kama hiki tulikuwa na pointi tisa tu, msimu huu mpaka sasa tuna pointi 19 hadi kumaliza mzunguko kwa kwanza, kwa maana hiyo hatujaharibu sana, tumefanya vizuri ila tunatakiwa kukaza kamba.

Golikipa wa timu hiyo yenye maskani yake mkoani Kigoma, Erick Johora, alitabiri kuwepo kwa ugumu zaidi mzunguko wa pili hasa mechi za ugenini.

"Mzunguko wa pili tunatarajia kuwa utakuwa mgumu sana, itakuwa kupata ushindi ugenini au pointi moja haitokuwa kazi rahisi, lakini sisi Mashujaa tutapambana," alisema kipa huyo.

Timu hiyo imemaliza mechi zake 15 za mzunguko wa kwanza ikiwa nafasi ya saba, ikikusanya pointi 19, ikishinda mechi nne, sare saba na kupoteza michezo minne.

## ZISIKUPITE

### NKUNKU ATAKIWA BARCA

WAKALA wa mshambuliaji wa Chelsea, Christopher Nkunku amesema mchezaji huyo mwenye miaka 22 anawaniwa na miamba ya Hispania, Barcelona. ***(Sport)***

### AMORIM HANA SHINIKIZO

KOCHA wa Manchester United, Ruben Amorim hana shinikizo la kumchagua mshambuliaji wa England Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 27, hata kama kukosekana kwake kunaweza kudhoofisha nafasi yao ya mazungumzo kuhusu kuuzwa kwake Januari. ***(ESPN)***

### TONALI HAKIELEWEKI N'CASTLE

NEWCASTLE United inaweza kusitasita kufikiria ofa kwa kiungo wa kati wa Italia, Sandro Tonali mwenye umri wa miaka 24, msimu ujao ili kutimiza sheria za faida na uendelevu, huku Juventus wakivutiwa. ***(Football Insider)***

### BAYERN YAMTAKA GITTENS

KLABU ya Bayern Munich inafikiria kumnunua winga wa Borussia Dortmund, Jamie Gittens mwenye umri wa miaka 20. ***(Sky Germany)***

### HAKUNA OFA KWA CHILWELL

CHELSEA haijapokea ofa yoyote kwa beki wao wa kushoto, Ben Chilwell mwenye umri wa miaka 28 ambaye amecheza mara moja pekee msimu huu kwenye Kombe la Carabao. ***(Sun)***

### RATEGUI ATUMIWA MASKAUTI

ARSENAL imetuma maskauti kumtazama mshambuliaji wa Atalanta mwenye umri wa miaka 25, Mateo Retegui. ***(Sportsport)***

### HARNANDEZ KUONDOKA MILAN

MVUTANO kati ya kocha wa AC Milan, Paulo Fonseca na mlinzi wa Ufaransa, Theo Hernandez unaweza kusababisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 kuondoka San Siro huku Real Madrid na Manchester United wakimtaka beki huyo wa kushoto. ***(Gazzetta dello Sport)***

### GODFREY KWA MKOPO SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inawania kumsajili beki wa Atlanta na England, Ben Godfrey mwenye umri wa miaka 2, kwa mkataba wa mkopo wa muda mfupi. ***(Football Insider)***

### UMTITI KUSITISHIWA MKATABA

KLABU ya Lille inaweza kusitisha mkataba wa beki wa Ufaransa, Samuel Umtiti mwenye umri wa miaka 31 ambaye hajacheza tangu Januari 2024 kwa sababu ya jeraha la goti. ***(Fichajes)***

### LUIS DIAZ HATAKI KUHAMA

LICHA ya uvumi fowadi wa Liverpool, Luis Diaz mwenye umri wa miaka 27 ana furaha kuendelea kucheza Anfield na hataki kuhama. ***(Sky Germany)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BUKAYO SAKA PIGO KUBWA ARSENAL

●●●Kocha Arteta amethibitisha nyota huyo atakuwa nje ya uwanja kwa...

**LONDON, England**

Arsenal imepata pigo kubwa baada ya kocha Mikel Arteta kuthibitisha kuwa winga Bukayo Saka atakuwa nje ya uwanja kwa „wiki nyingi" kutokana na kuchanika nyama za paja.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 aliambiwa habari hiyo baada ya kuonana na daktari maalumu, baada ya kuondoka uwanjani kwa magongo kwenye ushindi wa washikabunduki hao wa 5-1 dhidi ya Crystal Palace wikendi iliyopita.

„Haionekani vizuri," alisema Arteta. „Atakuwa nje kwa wiki nyingi."

"Ni pigo kubwa. Ni dhahiri ni mchezaji mkubwa kwetu, lazima tuone mchango aliokuwa nao kwenye timu. Litakuwa zoezi zuri sana kwetu kufikiria njia za kushinda changamoto nyingine.

"Ninaweka mawazo pamoja. Bado sijafika huko. Lakini nina mechi. Kisha nataka kuzungumza na wachezaji pia kuelewa ni jinsi gani tutatengeneza hilo na kulichukulia kwa njia chanya.

"Kiwango chake cha nishati, lugha yake ya mwili, na jinsi anavyowasiliana na timu nyingine lazima iwe nzuri sana kwa sababu ndiyo njia pekee ambayo anaweza kusaidia kwa sasa, kwa hiyo ni bora kufanya hivyo."

Ingawa Arteta alikuwa na nia ya kupata mbadala wa ndani, habari kwamba Raheem Sterling pia atakuwa nje ya uwanja kutokana na jeraha la goti ni pigo zaidi ikizingatiwa kuwa mchezaji huyo wa Chelsea ambaye yupo kwa mkopo angekuwa mbadala wa wazi.

"Atakuwa nje kwa wiki naamini," aliongeza Arteta. „Anahitaji kupimwa zaidi ili kufahamu ukubwa wa jeraha lake. Ni goti lake. Tunapaswa kusubiri na kuona saa nyingine 24. Kwa bahati mbaya atakuwa nje kwa muda."

HABARI MICHEZO

## Inzaghi hana tatizo na ukame wa Martínez

**MILAN, Italia**

KOCHA wa Inter Milan, Simone Inzaghi alipongeza ushindi wa mabao 2-0 wa timu yake kwenye Serie A nyumbani dhidi ya Como Jumatatu na akasema hana wasiwasi kuhusu ukame wa mabao wa nahodha wake, Lautaro Martínez.

Martinez hajafikia kiwango ambacho kilimfanya kuwa kinara wa mabao kwenye ligi msimu uliopita na ameshindwa kufunga kwa zaidi ya mwezi mmoja tangu kupata ushindi wa 1-0 dhidi ya Venezia mapema Novemba.

Hata hivyo, Inzaghi bado ana imani na fowadi wake, akisema raia huyo wa Argentina ana jukumu muhimu katika ratiba iliyojaa ya timu yake.

„Nilikuwa mshambuliaji, najua nyakati hizi hutokea," alisema.

„Lautaro alikuwa mmoja wa wachezaji bora dhidi ya Lazio.

„Washambuliaji wanafanya kazi kwa bidii, tunahitaji mengi kutoka kwao na tunajaribu kuwapumzisha iwezekanavyo.

„Nilimwambia Lautaro apumzike, kwa sababu amekuwa akifunga mabao kila mara, bahati itageuka na anapaswa kutokuwa na wasiwasi ikiwa hatapata nafasi za kufunga."

## Mourinho awaondoa wasiwasi mashabiki kwa upasuaji

**LISBON, Ureno**

JOSE Mourinho amewaambia mashabiki kuwa yuko vizuri baada ya kuibuka taarifa kuwa kocha huyo wa Fenerbahce atafanyiwa upasuaji nchini Ureno kutokana na tatizo la kiafya.

Kwa mujibu wa ripoti, Mourinho mwenye umri wa miaka 61, ataondolewa nyongo wakati wa likizo ya Krismasi kwa upasuaji nchini Ureno.

Kocha huyo wa zamani wa Chelsea, Manchester United na Real Madrid alichapisha video kwenye Instagram na kusema: „Heri ya Krismasi na asante sana kwa ujumbe mwingi."

Mourinho, ambaye aliongoza Fenerbahce katika sare ya 1-1 Ijumaa huko Eyupspor kabla ya mapumziko ya Krismasi, hakuingia kwa ndani kuzungumzia upasuaji huo, lakini alisema ni mdogo.

Aliandika: „Kwa wale ambao mmeonesha wasiwasi, ninaweza kuthibitisha taarifa za upasuaji wangu zimetiwa chumvi sana, ni utaratibu wa haraka na mdogo. Nitarejelea mazoezi siku ya kwanza nikirudi kutoka likizo, kama kawaida."

Fenerbahce watarejea dimbani Januari 5, watakapowakaribisha Hatayspor.

Mourinho alisema haitakuwa „kipindi cha furaha" kwake na sio kwa sababu ya upasuaji lakini kwa sababu alisikitishwa na mchezo wa mwisho wa timu yake mwaka huu.

Matokeo ya Ijumaa yameiacha Fenerbahce ya pili kwenye Super Ligi, pointi nane nyuma ya viongozi Galatasaray.

"Tutakuwa na siku chache za mapumziko lakini haitakuwa wakati wa furaha kwangu," alisema Mourinho.

„Kwa kweli, ningependelea kutokuwa na wakati huu wa mapumziko lakini tuliwaahidi wachezaji muda mrefu uliopita. Wachezaji wengi hawakuweza kuchukua zaidi ya siku 10 za mapumziko. Kwa hivyo, hii ilikuwa hali muhimu kwao kupumzika. Tunapaswa kufanya vizuri zaidi."



# FERNANDEZ: SASA NARUDI KWENYE UBORA WANGU

**LONDON, England**

ENZO Fernandez amekiri kuwa hajawa kwenye kiwango bora katika klabu ya Chelsea lakini ana matumaini ya kufanya vizuri baada ya kuanza vyema chini ya kocha Enzo Maresca.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina alikuwa mchezaji ghali zaidi wa Ligi Kuu England wakati Chelsea ilipomsajili kutoka Benfica kwa dili la euro milioni 121 siku ya mwisho ya usajili Januari 2023.

Baada ya miezi sita ya kwanza ya kuvutia pale Stamford Bridge, Fernández hakuwa tena kwenye ubora wake katika msimu wake wa kwanza kamili msimu uliopita baada ya kucheza sehemu kubwa ya kampeni akisumbuliwa na ngiri.

Fernández aliiambia ESPN, "Nilipofika ilikuwa ngumu sana, mwaka wa kwanza na nusu hapa, mabadiliko ya makocha, klabu haikuwa ikifanya vizuri na majeraha kibinafsi."

Fernandez mwenye umri wa miaka 23, alisema hakuwahi kuhisi shinikizo kutokana na bei iliyompeleka Chelsea.

„Haikuniathiri," alisema. „Nilijaribu kuwajibika bila shinikizo. Sikuridhika na nilichokuwa nikionesha, kisha nikajeruhiwa, mambo mengi mabaya yalitokea, nilijaribu kusonga mbele lakini leo najisikia vizuri sana, kama vile timu na tunatarajia kuendelea katika njia hii."

Maresca alichukua nafasi ya Mauricio Pochettino kama kocha msimu wa majira ya joto baada ya kuiongoza Leicester kupanda daraja msimu uliopita.

HABARI MICHEZO

# FOUNTAIN GATE YAPANIA KUMALIZA MWAKA KIBABE

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Fountain Gate imewaita mashabiki wa soka mkoani Manyara kujitokeza kwa wingi leo kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, kushuhudia mchezo wa mwisho kwa timu hiyo mwaka huu 2024, itakapocheza dhidi ya Namungo FC huku wakiahidi kuwapa furaha ya ushindi.

Ofisa Habari wa timu hiyo, Issa Mbuzi, amesema kuwa wataingia uwanjani leo siku ya Krisimasi kucheza mchezo wa mwisho kwa mwaka huu dhidi ya Namungo kwani baada ya hapo hawatocheza tena mchezo wowote wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwenye uwanja huo mwaka huu, badala yake watakwenda kumalizia kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam dhidi ya Yanga, Jumapili ijayo, Desemba 29.

„Leo ni mtoko, sikukuu ya Krismasi, mashabiki wa soka Babati na mkoa mzima wa Manyara, wanatakiwa kujitokeza kwa wingi kushuhudia mchezo wa mwisho kabisa kwa timu yao, kwa sababu baada ya hapo wataiona tena mwakani, mchezo unaofuata tutacheza Jumapili ijayo Dar es Salaam dhidi ya Yanga, kwa hiyo wajitokeze na familia zao kuja kuishangilia timu yetu na sisi tumeshaongeza na benchi la ufundi na wachezaji wengi ili wapambane kufa na kupona kuwapa furaha mashabiki wetu,“ alisema Mbuzi.

Alisema mbali na kusaka ushindi kwa ajili ya kuongeza mtaji wao kwenye msimamo wa Ligi Kuu, lakini wanataka kuweka rekodi ya kumaliza msimu kwenye uwanja wao kwa ushindi.

„Haiwezekani tumalize mwaka kwenye uwanja wetu kwa kipigo, au sare, hii itawanyong'onyesha mashabiki wetu ambao watakuwa wameacha kwenda kwenye burudani zingine kuja kutushangilia, halafu watoke na huzuni, hatutaki hilo litokeaa,“ alisema.

Fountain Gate itaingia kwenye mchezo wa leo ikiwa kwenye nafasi ya sita ya msimamo wa Ligi Kuu, ikikusanya pointi 20 mpaka sasa.

Inacheza na Namungo ambayo inakamata nafasi ya 12 kwenye msimamo wa ligi, ikiwa na pointi 14 kibindoni.



Vijana wa kituo cha michezo cha Jakaya Kikwete, wakiwania mpira wakati walipokuwa wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Kituo hicho jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Medo amwita Adam Adam Kagera

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kupokea kipigo cha mabao 5-2 dhidi ya Simba, Jumamosi iliyopita kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa kwenye uwanja wa Kaitaba, Kagera, Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Melis Medo amewaambia mabosi wa timu hiyo kuwa anamhitaji straika Adam Adam, ili aongeze nguvu kwenye safu ya ushambiliaji.

Mbali na straika huyo ambaye alisajiliwa msimu huu na Azam FC akitokea Mashujaa FC, Medo amewaambia wajiri wake kuwa anahitaji kipa wa kusaidiana na Ramadhani Chalamanda na Said Kipao, na mastraika wawili wenye ubora mkubwa ili kukifanya kikosi chake kuwa imara.

„Unaona tumefungwa na Simba kwa sababu ya uzoefu tu, tuna wachezaji ambao si wazoefu sana kwenye mikiki ya ligi, hata kama tusiwe na wachezaji wenye ubora kama wa Simba, Yanga na Azam, lakini angalau wawe wenye uzoefu, kwa maana hiyo tunaangalia dirisha la usajili tuone nini tutafanya, tutaongeza aina hiyo ya vijana,“ alisema kocha huyo.

Taarifa zinasema kwenye nafasi zote kocha huyo hajataja majina ya wachezaji zaidi ya Adam, ambaye amesema kama inawezekana kumchukua kutoka Azam basi waangalie uwezekano huo.

Habari zinasema kuwa tayari viongozi wa Kagera Sugar wameanza mazungumko na Azam FC kuangalia uwezekano wa kumpata straika huyo kwa mkopo.

Kwa sasa amekuwa hana wakati mzuri tangu aliposajiliwa na Azam, lakini mabao yake yaliisaidia sana Mashujaa FC msimu mmoja uliopita na kuifanya ibakie Ligi Kuu.

Timu hiyo imecheza michezo 15 na kumaliza mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu ikiwa imeshinda michezo miwili, sare tano na kupoteza mechi nane, ikifunga mabao 10 na kuruhusu nyavu zake kutikiswa mara 19 na inakamata nafasi ya 14 kwenye msimamo.

Kipigo cha mabao 5-2 ilichokipata dhidi ya Simba kimeifanya kuwa timu ya kwanza ya pekee mpaka sasa iliyoweka rekodi ya kupoteza mechi kwa idadi kubwa ya mabao kwenye michezo wa Ligi Kuu.

# Serengeti Boys yafuzu AFCON 2025

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Taifa ya Soka ya Tanzania chini ya miaka 17, Serengeti Boys imefanikiwa kufuzu kucheza fainali za Mataifa ya Afrika kwa umri huo zinazotarajiwa kuchezwa mwakani nchini Morocco baada ya kuifumua Sudan Kusini mabao 4-0 katika mchezo wa nusu fainali ya kusaka tiketi hiyo kwa ukanda wa CECAFA, uliochezwa jana mchana, Uwanja wa Nakivubo, Kampala, Uganda.

Mbali na kukata tiketi, Serengeti Boys pia imetinga hatua ya fainali ya michuano hiyo.

Mabao ya Serengeti Boys yalifungwa na Hussein Mbegu, Abel Joasiah na Ng'habi Zamu.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Agrrey Morris, ameelezea kufurahishwa kwake kuipeleka timu hiyo fainali, akisema hii ni mara ya kwanza kwenye historia yake ya soka.

**"Namshukuru Mungu, Watanzania wote, hili ni jambo kubwa sana kwangu kwa sababu ni mara ya kwanza kwenye historia yangu ya soka kuiwezesha timu ya Tanzania kufuzu, nimefurahi sana, ni jambo zuri kwangu, sasa naangalia mbele hatujajua tunacheza na nani fainali, lakini yoyote yule aje," alisema.**

Akuzungumzia mchezo huo alisema kuwa ulikuwa ni wa kimbinu zaidi na ndicho kilichofanya wapate ushindi huo.

"Ulikuwa ni mchezo wa kimbinu zaidi, tulisoma ubora na udhaifu wao na tukajua jinsi gani ya kukabiliana nao, kwa sababu wanapenda sana kushambulia, tukaweka wachezaji wawili wenye spidi ili tukitoka kwetu tuondoke kwa kasi na hii imetusaidia sana," alisema.

Alisema kwa sasa wanasubiri mchezo wa fainali kati ya wenyeji Uganda dhidi ua Somalia, akisema utakuwa mgumu na wenye mahitaji tofauti.

"Kila timu ina aina yake ya mchezo, kwa hiyo tunataka kuangalia ni timu gani itaingia fainali ili tujue namna ya kukabiliana nayo," alisema.

Uganda na Somalia pia zilitarajia kucheza jana katika mchezo wa pili wa nusu fainali.



Michezo
Jumatano Desemba 25, 2024
Nipashe

# ‘UBAYA UBWELA’ WAIKUMBA JKT

## ●●●Ahou aihakikishia Simba kula Krismasi kileleni kwenye msimamo wa...

**Na Mwandishi Wetu**

BAO la dakika za majeruhi lililofungwa na kiungo mshambuaji raia wa Ivory Coast, Jean Ahoua, jana liliipa Simba ushindi wa bao 1-0 dhidi ya JKT Tanzania, katika mchezo mkali wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliopigwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

Wakati baadhi ya watazamaji wakiwa wameanza kuondoka, wengine wakiamini mchezo huo ungeisha kwa suluhu, yalitokea makosa mawili kwa wakati mmoja ndani ya eneo la hatari la JKT Tanzania na mwamuzi wa mchezo huo kuamuru mkwaju wa penalti uliokwenda kukwamishwa wavuni na kiungo huyo na kufikisha idadi ya mabao saba mpaka sasa kwenye Ligi Kuu.

Wakati Edson Katanga akionekana kuushika mpira kwenye eneo la hatari, wakati huo, Mohamed Bakari alimzuia kwa kutumia mikono Shomari Kapombe ambaye alikuwa anaifuata krosi iliyopigwa upande wa kushoto wakati wachezaji wa Simba walipokuwa wakifanya mashambulizi mfululizo langoni mwa wapinzani wao kwa dakika 10 za mwisho.

Bakari alizawadiwa kadi ya njano kwa faulo hiyo, lakini kwa sababu alikuwa ameshapewa kadi ya njano awali, akaonyeshwa tena nyekundu.

Ushindi wa jana ni wa nane mfululizo kwa timu hiyo kwenye Ligi Kuu, tangu ilipofungwa na Yanga bao 1-0, Oktoba 19 mwaka huu.

kwa sasa Simba wamefikisha pointi 37 na kuzidi kujichimbia juu ya kilele cha msimamo wa ligi ikiwa imeshacheza michezo 14 na kusalia mchezo mmoja kumaliza mzunguko wa kwanza.

Katika mechi ya jana haikuwa rahisi kwa Simba kufanya kama inavyofanya siku zote, kwani ilikabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa wapinzani wao walioonekana kuziba mianya yote na kushambulia kwa kushtukiza.

Mabadiliko yaliyofanywa kipindi cha pili na Kocha Mkuu, Fadlu Davids, kwa kuwaingiza Josehua Mutale, Mohamed Hussein Tshabalala, Jean Ahoua na Steven Mukwala, yalionekana kuipa Simba uhai na kushambulia kwa kasi tofauti na mwanzo.



Mshambuliaji wa Simba, Ladaki Chasambi (kulia), akimtoka mchezaji wa JKT Tanzania, Najim Magulu kwenye mchezo wa Ligi Kuu uliochezwa jana Uwanja wa KMC, Dar es Salaam. Simba ilishinda bao 1-0. **PICHA: SIMBA**

Ahoua kwa kiasi kikubwa alionekana kubadilisha zaidi mchezo kwani alionekana hatari zaidi kila anaposhika mpira, akishambulia kwa kasi, mashuti makali na pasi zake za hatari.

Hata hivyo, golikipa wa JKT Tanzania, Yakoub Selemani ndiye alikuwa shujaa kwa timu hiyo kwani aliokoa michomo mingi ya hatari langoni mwake.

Leonel Ateba ndiye aliyekosa mabao mengi kipindi cha kwanza katika mchezo wa jana.

Simba ilianza kuwashambulia maafande kwa faulo ya dakika ya saba iliyopigwa na Valentine Nouma karibu kabisa na lango la JKT Tanzania, mpira uliwababatiza mabeki na kuzua kizaazaa langoni huku wachezaji wa Simba wakichelewa kuukwamisha wavuni.

Simba ilifanya shambulio lingine dakika ya 16, pale krosi ya Elie Mpanzu ilipopanguliwa na kipa, Yakoub.

Dakika moja baadaye kipa huyo alifanya kazi ya ziada, aliporuka juu na kuupiga ngumi mpira wa kichwa uliopigwa na Leonel Ateba, akiunganisha krosi kutoka kwa Nouma hata hivyo mpira ulitoka nje na kuwa kona ambayo haikuwa na madhara.

JKT Tanzania ilipiga hodi kwenye lango la Simba dakika ya 21, pale Hassan Kapalata alipopata mpira akiwa pembeni kidogo ya lango, shuti lake kali lililoka sentimeta chache langoni.

Ateba aliruka ‚tik-tak‘ dakika ya 22, kuunganisha krosi ya Kapombe, lakini aliukosa mpira na kuokolewa kwenye eneo la hatari.

Hassan Nassor, nusura aipatie JKT Tanzania bao dakika ya 28, alipounganisha kwa kichwa faulo iliyopigwa na Shiza Kichuya, akiwa hajawekewa ulinzi na mabeki wa Simba, bahati mbaya ukatoka nje kidogo la lango.

Mpanzu alilitia msukosuko lango la JKT Tanzania dakika ya 39, baada ya faulo aliyopiga kuvuka ukuta, lakini kipa Yakoub ambaye alifanya kazi kubwa jana, aliruka upande wake wa kulia na kupangua mpira kwa ustadi mkubwa.

## Yanga yawaandalia ‘Wananchi’ zawadi Krismasi

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, amesema wamekwenda jijini Dodoma kwa lengo moja tu, kuwapa zawadi ya sikukuu ya Krismasi wananchi na mashabiki wa timu hiyo kwa ushindi leo dhidi ya Dodoma Jiji FC.

Yanga leo itashuka dimbani saa 10:00 jioni kucheza dhidi ya wenyeji wao, kwenye Uwanja wa Jamhuri katika kampeni yake ya kutaka kutetea taji lake la ubingwa, ikitaka kulichukua kwa mara ya nne mfululizo.

Mjerumani huyo amesema ushindi wowote watakaoupata utakuwa ni muhimu kwao kwani utawapa pointi tatu na kuzidi kuelekea juu ya msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

„Tumekuja hapa kwa lengo moja, tuchukue pointi tatu na kuwapa zawadi ya Krismasi mashabiki wetu, hili ndiyo jambo muhimu kwetu,“ alisema kocha huyo.

Hata hivyo, alisema huenda akakibadilisha kidogo kikosi chake kutokana na kuhofia uchovu wa wachezaji wake ambao wametumika kwenye michezo miwili mfululizo waliyocheza.

“Itakuwa mechi ngumu kwa sababu tumecheza michezo miwili mfululizo ndani ya muda mfupi, kwa hiyo tunahitaji pia kufanya mabadiliko ya kikosi,“ alisema.

Alhamisi iliyopita Yanga ilicheza mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Mashujaa FC na kushinda mabao 3-2, Jumapili iliyopita ikaingia tena dimbani kupepetana na Prisons, ikishinda mabao 4-0, mechi zote zikipigwa, Uwanja wa KMC, Dar es Salaam.

“Nimefika hapa kama wiki tatu zilizopita, nimekutana na michezo mfululizo bado sijapata muda wa kukaa na vijana wangu kuwapa mazoezi ya kutosha, kuwaelekeza kwa utulivu kile ninachokihitaji, pia kuwafanya wachezaji wote wawe na utimamu wa mwili, nadhani baada ya wiki nne au tano hali itabadilika kabisa,“ alisema kocha huyo aliyetwaa nafasi ya Miguel Gamondi.

Mchezo wa leo utakuwa wa 14 kwa Yanga ambayo ina pointi 33, ikiwa imeshinda michezo 11, ikipoteza miwili, mabao 23 ya kufunga na imeruhusu mabao sita na haijatoka sare yoyote mpaka sasa.

Ipo kwenye nafasi ya pili ya msimamo ikiwa kwa uwiano mzuri wa mabao ya kufunga na kufungwa dhidi ya Azam FC ambayo nayo ina pointi 33 ikiwa nafasi ya tatu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >